JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU
# IDARA YA MENEJIMENTI YA MAAFA

# MPANGO MKAKATI WA TAIFA WA AFYA MOJA
# (2022 – 2027)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

IDARA YA MENEJIMENTI YA MAAFA

# MPANGO MKAKATI WA TAIFA WA AFYA MOJA (2022 – 2027)

## DIBAJI



Matishio ya hivi karibuni ya majanga ya kimataifa ya milipuko ya magonjwa yametokana na athari zinazoongezeka za vimelea vya magonjwa ambukizi kwa afya ya binadamu na wanyama. Imedhihirika pia kuwa mabadiliko katika mazingira, ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa shughuli za kilimo, ongezeko la watu, ukuaji wa miji, mabadiliko ya tabianchi na kupanuka kwa shughuli za binadamu katika makazi ya wanyamapori ni vichocheo vya milipuko ya magonjwa haya ambukizi kwa wanyama na wanadamu (zuonotiki). Mbinu ya Afya Moja imetambuliwa kama mkakati mkuu wa kudhibiti na kuzuia magonjwa, kwani inasisitiza uhusiano wa afya ya binadamu, wanyama na mazingira pamoja na umuhimu wa juhudi za pamoja za kudhibiti matishio ya milipuko ya magonjwa mapya na yale yanayojirudia. Hili limejidhihirisha katika mlipuko wa hivi karibuni wa janga la Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO -19) nchini Tanzania mwaka 2020, ambapo kuimarishwa kwa mawasiliano na ushirikiano wa kisekta wakati wa mlipuko huo kulisababisha kushughulikiwa kwa ufanisi tukio la mlipuko huo. Juhudi kama hizo zilionekana pia hapo kabla katika utayarishaji wa waraka wa pamoja wa Kitaifa wa Mpango wa Dharura wa Kujiandaa na Ugonjwa unaovuka mipaka wa Mafua Makali ya Ndege na Mafua ya Binadamu mwaka 2006 na mikakati inayolenga kuzuia na kudhibiti magonjwa ya zuonotiki yaliyopewa kipaumbele kama ilivyoelezwa katika Mpango Mkakati wa Kwanza wa Kitaifa wa Afya Moja wa mwaka 2015/2020.

Huu ni "Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Afya Moja" wa pili kuandaliwa kwa mbinu ya ushirikishwaji wa sekta mbalimbali. Mpango umechukua na kuzingatia utaalamu kutoka sekta hizo, na unaakisi dhamira ya pamoja ya kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya afya ya binadamu, mifugo, wanyamapori na mazingira ili kupunguza milipuko ya magonjwa ambukizi (zuonotiki), usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matishio mengine ya afya ya jamii. Uratibu wa uendelezaji wa mpango huu ulifanyika chini ya Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Mpango Mkakati huu ni waraka elekezi wa Serikali nzima unaolenga kuweka muhtasari wa shughuli na operesheni miongoni mwa wadau mbalimbali. Mpango huu pia unalenga kuunda na kudumisha ushirikiano kati ya sekta za kuzuia na kudhibiti magonjwa ambukizi kati ya binadamu na wanyama (zuonotiki), usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na matishio mengine ya afya ya jamii ili kuhakikisha kuwa kuna mwendelezo wa maandalizi na mwitikio wa haraka kwa wakati unaofaa na majibu thabiti yaliyoratibiwa katika kuibuka kwa tukio au janga lolote. Utekelezaji na mafanikio ya Mpango Mkakati huu yatachangia kwa kiasi kikubwa kuboresha lengo la jumla la afya ya jamii, usalama na ulinzi wa chakula, na maisha ya watu wote.

Katika kuzingatia masuala haya, tunatoa wito kwa idara nyingine za Serikali, washirika wa maendeleo, taasisi za elimu ya juu, taasisi za utafiti, asasi za kiraia , sekta binafsi na jumuiya ya Watanzania kwa ujumla kuungana nasi katika kutekeleza mpango huu adhimu wa Afya Moja. Mpango Mkakati huu unapaswa kuzingatiwa kuwa ni "nyaraka hai" na uko wazi kwa maoni, nyongeza na marekebisho kulingana na mahitaji yanayobadilika.



Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)
**Waziri Mkuu**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

## SHUKURANI



Ofisi ya Waziri Mkuu inapenda kuwashukuru wote waliojitolea muda wao kuchangia kufanikisha kukamilika kwa Mpango Mkakati huu wa Utekelezaji wa Afya Moja nchini Tanzania.

Shukurani za pekee ziwaendee timu na wengine wote walioshiriki kufanya kazi hii ya kuandaa Mpango Mkakati huu bila kuchoka, wakiwemo kutoka: Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI); Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira; Wizara ya Afya ; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Kilimo; Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Wakala ya Maabara ya Mifugo Tanzania; Chuo Kikuu cha Dodoma; Mtandao wa Afya Moja katika Vyuo Vikuu Afrika (AFROHUN) na wawakilishi kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Washirika wa Maendeleo na Asasi Zisizo za Serikali (AZISE).

Aidha, tunapenda kulishukuru Shirika la Chakula na Kilimo Duniani na Programu ya Kimataifa ya Mpango wa Usalama wa Kemikali na Biolojia wa *Sandia National Laboratories* kwa kutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya marekebisho ya Mpango Mkakati huu muhimu.



Dkt. John A. K. Jingu
**Katibu Mkuu**
**Ofisi ya Waziri Mkuu**
**(Sera, Bunge na Uratibu)**

## YALIYOMO


Dibaji ..... ii
Shukurani ..... iii
Muhtasari ..... viii
1. Utangulizi ..... 1
1.1 Usuli ..... 1
1.2 Chimbuko la Afya Moja ..... 1
1.3.2 Muundo wa Kiutawala ..... 3
1.3.3 Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi ..... 3
1.4 Sekta za Kilimo, Mifugo na Wanyamapori ..... 3
1.5 Matishio ya Milipuko ya Magonjwa Yanayoibuka Duniani ..... 4
1.5.1 Magonjwa ya Zuonotiki ..... 5
1.5.2 Usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (AMR) ..... 5
1.5.3 Matishio ya Usalama wa Afya na Ulinzi wa Kibiolojia ..... 7
1.5.4 Matishio ya Usalama wa Chakula ..... 7
1.5.5 Matishio ya Afya ya Mazingira ..... 8
1.5.6 Matishio ya kiafya katika mabadiliko ya tabianchi ..... 8
1.5.7 Matishio ya kiafya kutokana na majanga yanayoibuka na yanayojirudia ..... 9
1.6 Mbinu ya Mfumo wa Afya Moja ..... 10
1.7 Mbinu ya Mfumo wa Afya Moja Tanzania ..... 10
1.8 Uratibu wa Afya Moja ..... 11
2. UCHAMBUZI WA HALI ILIYOPO ..... 12
2.1 Utekelezaji wa Kanuni za Afya za Kimataifa (IHR (2005)) ..... 12
2.2 Tathmini na Uboreshaji wa Mifumo ya Afya ..... 13
2.3 Mfumo wa Udhibiti ..... 13
2.4 Majukumu na Kazi za Sehemu ya Afya Moja ..... 15
2.5 Mfumo wa Afya ya Binadamu, Wanyama Na Mazingira Tanzania ..... 15
2.5.1 Wizara ya Afya ..... 15
2.5.2 Wizara ya Mifugo na Uvuvi ..... 16
2.5.3 Wizara ya Maliasili na Utalii ..... 17
2.5.4 Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ..... 19
2.5.5 Wizara ya Kilimo ..... 19
2.5.6 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ..... 20
2.6 Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto (SWOC) ..... 20
2.7 Uchambuzi wa Wadau ..... 28
3. MPANGO MKAKATI ..... 29
3.1 Kusudi ..... 29

3.2 Dira na Dhamira ........ 29
3.2.1 Dira ........ 30
3.2.2 Dhamira ........ 30
3.3 Malengo ya Mkakati ........ 30
3.4 Maadili ya Msingi........ 30
3.5 Kanuni Elekezi ........ 30
3.6 Nguzo ya Malengo Kimkakati........ 30
4. MFUMO WA KUTOA MATOKEO........ 65
4.1 Utangulizi ........ 65
4.2 Mlolongo wa Matokeo ........ 65
4.4 Ufuatiliaji na Tathimini ........ 71
4.4.1 Ufuatiliaji na Tathimini........ 71
4.4.2 Mpango wa Ufuatiliaji........ 71
4.4.3 Mpango wa Tathimini........ 71
4.5 Mpango wa kuripoti ........ 73
4.5.1 Mpango wa Ndani wa utoaji Taarifa........ 73
4.5.2 Mpango wa Nje wa utoaji Taarifa........ 73
4.6 Mapitio ya Mpango........ 74
Kiambatanisho 1: MPANGO MKAKATI WA TAIFA WA AFYA MOJA 2022 - 2027 MPANGO KAZI WA KILA MWAKA........76
Kiambatisho Na. 2: ORODHA YA WACHANGIAJI ........116

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali na 1: Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto (SWOC) ............ 21
Jedwali Na. 2: Matrikisi ya Matokeo ............ 31
Jedwali Na. 3: Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ............ 66
Jedwali Na. 4: Mpango wa Ndani wa kuripoti ............ 73
Jedwali Na. 5: Mpango wa Nje wa kuripoti ............ 73

## VIFUPISHO NA TAFSIRI ZAKE

| | |
|---|---|
| UVIKO -19 | Ugonjwa wa Virusi vya Korona |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| AZISE | Asasi Zisizo za Serikali |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| OWM | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |

## MUHTASARI

Mpango Mkakati huu umeandaliwa kwa mujibu wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2020, Mwongozo wa Upangaji Mkakati na Bajeti ya muda wa Kati wa mwaka 2021. Mbinu iliyotumika ilikuwa kupitia Mpango Mkakati wa Kwanza wa mwaka 2015-2020 ili kubainisha maeneo ya mafanikio, udhaifu, na vikwazo, kutafuta taarifa kutoka kwa watekelezaji wa Afya Moja na kuendesha mikutano shirikishi ya wadau wa Afya Moja ili kupokea maoni yao. Mpango Mkakati huu wa Afya Moja uliofanyiwa marekebisho kwa pamoja utaruhusu wataalamu katika sekta za afya ya binadamu, mifugo, wanyama pori, mazingira na wataalamu wa sekta nyingine kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuzuia, kutambua, kujiandaa na kukabili magonjwa yanayoibuka au kujirudia kutokana na mwingiliano.

Mpango Mkakati huu umegawanyika katika sura nne. Sura ya Kwanza inatoa utangulizi, usuli, asili ya Afya Moja, Maeneo ya Nchi yanayojumuisha jiografia na idadi ya watu wa Tanzania, Muundo wa utawala, Maendeleo ya kijamii na kiuchumi, Kilimo, Mifugo na Sekta za wanyamapori. Sura hiyo pia *inaelezea* matishio ya magonjwa yanayoibuka na yanayovuka mipaka ikizingatia Magonjwa yanayoweza kuwapata binadamu na wanyama (Zuonotiki), Usugu wa Vimelea dhidi ya dawa (AMR), Matishio ya Usalama wa Afya (biosafety) na Ulinzi wa Kiusalama wa afya (biosecurity), Matishio ya usalama wa chakula, Matishio ya afya ya mazingira, Matishio ya kiafya yanayohusisha mabadiliko ya tabianchi na Matisho mengine ya kiafya yanayoibuka upya au kujirudia. Utangulizi huo pia unahusu mtazamo wa Afya Moja duniani, nchini Tanzania pamoja na uratibu wake.

Sura ya Pili inahusu uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa Kanuni za Afya za Kimataifa (IHR) *za* Mwaka 2005; Tathmini na uboreshaji wa mifumo ya afya; Mfumo wa udhibiti wa majanga kwa pamoja, mamlaka na kazi za idara na sehemu ya Afya Moja zimeelezwa. Sura hiyo pia inafafanua Mifumo ya Afya ya Binadamu, Wanyama na Mazingira nchini Tanzania ambayo inajumuisha Wizara ya Afya ; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maliasili na Utalii; Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira; Wizara ya Kilimo; na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sura hii pia inaainisha Uwezo , Udhaifu, Fursa na Changamoto zilizotokana na tathmini ya utendaji na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Afya Moja wa mwaka 2015-2020. Aidha, sura hii inaeleza uchambuzi wa wadau katika Afya Moja.

Sura ya Tatu inaangazia Mpango Mkakati ambapo inaainisha Dira, Dhamira na Dhima, Maadili ya Msingi na Kanuni Elekezi. Vilevile, inaeleza nguzo sita za kimkakati ambazo ni Uratibu; Ufuatiliaji, Utambuzi, Kinga na Udhibiti; Maandalizi na Utayari wa kukabili matukio; Utafiti na maendeleo; Uhamasishaji, Utetezi na Mawasiliano pamoja na Mafunzo na Elimu. Kwa kila nguzo, kuna malengo ya kimkakati, lengo mahususi , shabaha, shughuli, viashirio na njia za uthibitishaji.

Sura ya Nne inaeleza mfumo wa matokeo kwa kuzingatia nguzo za kimkakati; ufuatiliaji na tathmini ya mkakati, mapitio ya mpango pamoja na mpango wa kutoa taarifa. Pia, mpango wa utekelezaji wa kila mwaka wa kukamilisha Mkakati wa Afya Moja *wa* mwaka 2022-2027 umewasilishwa kama kiambatisho na 1.

# 1. UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Kuibuka na kujirudia kwa janga na matishio mengine ya afya ya jamii ni suala lenye changamoto na lenye sura nyingi, kama ilivyodhihirishwa na mlipuko wa UVIKO - 19. Usimamizi na ukabilianaji wake kwa ufanisi unahitaji njia na hatua nyingi shirikishi na uratibu endelevu wa sekta mtambuko.

Mbinu ya Afya Moja ni mkakati uliobuniwa kukuza matumizi ya maarifa na ujuzi wa sekta na taaluma mbalimbali zikiwemo za kitabibu, afya ya jamii, mifugo na mazingira kushughulikia changamoto za afya ya wanyama, binadamu na mazingira.

Ingawa Afya Moja siyo dhana ngeni, lakini imekuja kuwa muhimu zaidi katika miaka ya hivi karibuni kwa lengo la kufikia kiwango cha hali ya juu cha afya bora kwa wanadamu, wanyama na mazingira.

Mwingiliano miongoni mwa binadamu, wanyama, na mazingira unaendelea kubadilika. Hali ya ongeeko la idadi ya watu na wanyama, mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya ardhi, na kuongezeka kwa safari na biashara za kimataifa hutoa fursa za kuenea kwa magonjwa. Takriban asilimia 75 ya magonjwa ya kuambukiza yaliyojitokeza hivi karibuni na kuathiri wanadamu kiasili ni magonjwa ya wanyama; aidha, asilimia 60 ya vimelea vya magonjwa yote ya binadamu hivi sasa inatokana na magonjwa yanayopatikana kwa mifugo. Afya Moja inajumuisha taaluma za afya, lakini pia inajumuisha wataalamu mbalimbali kwa mfano wataalamu wa wanyamapori, wanaanthropolojia, wachumi, wanamazingira, wanasayansi wa tabianchi na wanasosholojia. Afya Moja inatambua kwamba matatizo na changamoto zinazokabili afya ya binadamu,mnyama na mazingira zinaweza kutatulika vyema kwa njia ya mawasiliano na ushirikiano baina ya fani mbalimbali. Afya Moja inazidi kutambuliwa na taasisi za kitaifa na kimataifa kama njia mwafaka zaidi ya kushughulikia masuala changamano katika mazingira yanayowakutanisha wanyama nabinadamu.

## 1.2 Chimbuko la Afya Moja

Dhana ya Afya Moja ilitanguliwa na dhana ya 'Dawa Moja' ambayo ina mizizi ya Kiafrika tangu miaka ya 1960, mtaalamu wa epidemiolojia wa Kimarekani *Calvin Schwabe*, akiwa anafanya kazi yake na wafugaji wa Dinka nchini Sudan alianzisha neno 'Dawa Moja' kutokana na kufanana kwa dawa ya binadamu na ile ya mifugo. Katika miaka ya 1980, dhana ya 'Dawa Moja' ilibadilishwa na kupanuliwa kuwa 'Afya Moja' ili kuakisi dhana ya afya kwa mfumo mzima wa ikolojia kama ilivyoanzishwa na mashirika haya ya kimataifa: Shirika la Afya Duniani, Shirika la Chakula na Kilimo.

Barani Afrika, mbinu ya Afya Moja ilianza kutumika mwaka wa 2018 wakati programu ya Afya Moja ilipokubalika na Vituo vya Afrika vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (*Africa CDC*). Programu hii imezingatia masuala mtambuko ya afya ya jamii ikiwa ni pamoja na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawana magonjwa *ya* zuonotiki kama maeneo ya kipaumbele. Programu ya Afya Moja katika Kituo cha *Africa* CDC inajumuisha kikundi kazi cha wataalamu wa Afya *Moja* (OH-TWG) chenye mgawanyiko ulio na uwakilishi kutoka vitengo vitano vya kitaalamu ambavyo ni: ufuatiliaji na intelijensia ya magonjwa, maandalizi ya dharura na kukabiliana na

maafa, mifumo ya maabara, taasisi za afya ya jamii,utafiti, udhibiti na uzuiaji wa magonjwa.

Wakati wa Mkutano wa 35 wa Kawaida wa Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki uliofanyika mwaka 2017, iliamuliwa kwamba dhana ya Afya Moja itumiwe na mataifa hayo na Jukwaa la Afya Moja la Jumuiya ya Afrika Mashariki lianzishwe na kuwezeshwa kufanya kazi. Mnamo mwaka wa 2019, Baraza la 19 la Kisekta la Mawaziri wa Afya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki liliagiza Sekretarieti ya Jumuiya hiyo kuimarisha ushirikiano na uratibu wa sekta mbalimbali kwa kuanzisha Mkakati wa Afya Moja wa kikanda. Inatarajiwa kwamba kupitishwa kwa mkakati huu kutatoa mwongozo wa utayari wa fani na sekta mbalimbali katika kujiandaa, kuzuia, kutambua na kukabiliana na matishio ya afya ya jamii katika mipaka ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na hatimaye kuboresha uratibu katika kukabiliana, kuzuia na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza yanayohusiana na Afya Moja kwa wanadamu, wanyama na mazingira.

Nchini Tanzania, dhana ya Afya Moja, imeungwa mkono na sekta mbalimbali, na ilikubaliwa kwa mara ya kwanza katika udhibiti wa mlipuko wa Homa ya Bonde la Ufa mwaka 2007. Katika kipindi *hicho*, idadi ya mitandao na majukwaa ya Afya Moja yaliundwa. Haya ni pamoja na Kituo cha Kusini mwa Afrika cha kufuatilia Magonjwa ya Kuambukiza (SACIDS), Mtandao wa Afya Moja wa Afrika ya Kati na Mashariki (OHCEA), Muungano wa Utafiti wa Kiafrika wa Mfumo wa Mazingira na Afya ya Idadi ya Watu (*AfriqueOne*) *na* Mitandao ya Kitaifa ya Afya Moja ya Utafiti iliyoimarishwa ya Magonjwa ya Kuambukiza (*NRN-Biomed*), Kikosi Kazi cha usistisekosi (*Cysticercosis*) katika Afrika Mashariki na Kusini (*CWGESA*) na Afya kwa Wanyama na Maisha (HALI). Mitandao hii na majukwaa mengi yalianzishwa *kwa* ushirikiano na wanasayansi wa utafiti katika vyuo vikuu na taasisi za utafiti ili kukuza utafiti wa Afya Moja na kutoa uthibitisho kwa watunga sera. Ajenda ya Kitaifa ya Afya Moja nchini Tanzania ilibuniwa na kurasimishwa wakati wa Mkutano wa Pili wa Wanasayansi wa Afya Moja pamoja na Taasisi ya Utafiti wa magonjwa ya Binadamu (NIMR) uliofanyika mwaka 2013.

## 1.3 Sura ya Nchi

### 3.1.1. Jiografia na Idadi ya watu Tanzania

Tanzania ni nchi ya Afrika Mashariki katika Ukanda wa Maziwa Makuu, inayojumuisha jumla ya eneo la maji na nchi kavu lenye kilometa za mraba 947,303, ambapo kilometa za mraba 886,040 zinajumuisha ardhi na kilometa za mraba 62,050 zinajumuisha maji (Lake , 2013).

Hali ya hewa inatofautiana kulingana na kanda za kijiografia: kitropiki kwenye pwani ambapo ni joto na unyevu (msimu wa mvua Machi - Mei); halijoto katika milima yenye mvua fupi inayonyesha kati ya Novemba-Desemba na mvua ndefu inayonyesha kati ya Februari-Mei, wakati eneo la uwanda wa nyanda lina halikavu na tofauti kubwa za msimu wa joto. Mvua hunyesha vyema mwaka mzima kufikia kilele chake katika kipindi cha Machi hadi Mei. Hali ya hewa kama hii anuwai inawezesha vimelea mbalimbali vya magonjwa kuathiri afya ya mifugo na afya ya jamii. Jumla ya wakazi wa Tanzania wakati wa sensa ya mwaka 2022 ilikuwa 61,741,120, huku msongamano ukitofautiana kutoka 12/$km^2$ katika mikoa yenye wakazi wachache, kama vile Katavi, hadi 3,133/ $km^2$ katika mikoa yenye wakazi wengi, kama vile Dar es Salaam (Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2022).

Kiwango cha jumla cha ukuaji wa idadi ya watu kinakadiriwa kuwa asilimilia 2.9 kwa mwaka huku kasi ya ukuaji wa miji ikifikia asilimia 4.77 kwa mwaka. Kilimo kinasaidia maisha ya asilimia 82 ya watu, asilimia 70 wakiwa vijijini (Ripoti ya Taifa, Dar es Salaam, Ofisi ya Waziri Mkuu, 2007/2008). Takriban asilimia 37 (1,745,776 kati ya 4,901,837) ya kaya zinafuga mifugo.

#### 1.3.2 Muundo wa Kiutawala

Tanzania imegawanywa katika mikoa 31 ya kiutawala: 26 kwa Bara na mitano Zanzibar (tatu Unguja, miwili Pemba). Kuna wilaya 169, zinazojulikana kama mamlaka za serikali za mitaa. Tangu mwaka 1986, serikali imepitia mageuzi kadhaa katika sekta zake, zikiwemo za Umma, Kilimo na Serikali za Mitaa. Sekta zinazohusika katika shughuli za Afya Moja hufanya kazi katika ngazi ya Taifa na ya Serikali za Mitaa. Ndani ya utawala uliogatuliwa, huduma za mifugo zinasimamiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Huduma ya afya ya jamii inasimamiwa na Wizara ya Afya katika ngazi ya Taifa na ngazi ya Mkoa, na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) *na* huduma ya wanyamapori inasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

#### 1.3.3 Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi

Pato la Taifa linaonesha ukuaji wa wastani wa takriban asilimia 6.5 - 7 kati ya 2016 na 2020, na wastani wa mfumuko wa bei wa kila mwaka wa asilimia 3.3 . Kwa mujibu wa Mpango wa sasa wa Maendeleo wa Miaka Mitano [*FYDP III*], wastani unaolengwa wa ukuaji wa Pato la Taifa unatarajiwa kuwa si chini ya asilimia 8 kwa mwaka. Msukumo wa ajenda ya maendeleo ya Tanzania umekuwa katika ukuaji wa uchumi na hasa kushughulikia athari mbaya za kutojua kusoma na kuandika, umaskini na magonjwa. Miongoni mwa mambo yanayochangia kutofikia malengo yaliyokusudiwa ni pamoja na; mabadiliko ya tabianchi yakiwemo mafuriko yanayoathiri miundombinu; mlipuko wa magonjwa ikiwa ni pamoja na (UVIKO - 19) ambayo huathiri biashara na uwekezaji; uzalishaji mdogo na ukuaji mdogo wa sekta za msingi.

### 1.4 Sekta za Kilimo, Mifugo na Wanyamapori

Tanzania ina hekta milioni 95.5 za ardhi, ambapo hekta milioni 44 zimeainishwa kuwa zinafaa kwa kilimo. Hata hivyo, pamoja na uwezo huu, ni hekta milioni 10.6 pekee ndizo zinazotumika kwa sasa kwa ajili ya uzalishaji wa mazao. Ingawa hekta milioni 50 za nyanda za malisho zinafaa kwa malisho ya mifugo, ni asilimia 50 tu ndizo zinazotumika. Pamoja na hayo, sekta ya kilimo imeendelea kutumika kama tegemeo la maisha ya vijijini na usalama wa chakula wa Taifa. Hakika, sekta hii inasaidia maisha ya karibu asilimia 82 ya watu. Sekta hii bado ina sifa ya mifumo ya wakulima wadogo na wa jadi. Utendaji wa sekta pia unaathiriwa vibaya na kuendelea kwa matumizi ya chini ya rasilimali za kijenetiki; wadudu waharibifu na magonjwa; ufugaji duni na huduma duni za ugani, pamoja na mifumo duni ya uhamishaji wa teknolojia. Mambo mengine yanahusiana na uwezo dhaifu ambao ni pamoja na mifumo ya kuongeza thamani na ya masoko, athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi na mifumo duni ya matumizi ya ardhi.

Tanzania ina idadi ya ng’ombe milioni 35.3, mbuzi milioni 25.6, kondoo milioni 8.8, mbwa milioni 4, nguruwe milioni 3.4 na punda 657,389. Aidha, idadi ya kuku ni milioni 92.8 ambapo kuku wa asili ni milioni 42.7 na kuku wa kisasa ni milioni 50.1. Pamoja na kutoa bidhaa za chakula, mifugo ina jukumu kubwa kama injini ya maisha na maendeleo katika maeneo ya vijijini. Mifugo hutumika kama nguvu kazi, usafiri na

hutoa samadi inayotumika kama mbolea kwa shughuli za kilimo cha mazao na vyanzo vya nishati vinavyowezekana kupitia teknolojia ya biogesi.

Zaidi ya hayo, Tanzania ina asilimia 20 ya spishi za wanyama wakubwa barani Afrika, wanaopatikana katika hifadhi zake, zilizotawanyika katika eneo la zaidi ya 42,000 km2 na kutengeneza takriban asilimia 38 ya eneo la nchi. Mwingiliano huu kati ya wanadamu, wanyama na mazingira, unatoa fursa kwa wote ya kuchangia rasilimali nyingi zilizopo lakini pia ni chanzo cha magonjwa yanayoathiri afya na ustawi wa jamii na uchumi wa binadamu (WHO 2020).

### 1.5 Matishio ya Milipuko ya Magonjwa Yanayoibuka Duniani

Hivi karibuni, mataifa duniani kote yamekuwa yakikabiliana na ongezeko la magonjwa yanayoibuka na kujirudia kutokana na mwingiliano wa wanadamu, wanyama na mazingira.Vimelea vya magonjwa haya yanayohusika na kuibuka au kujirudia vinaweza kuenea kwa haraka, siyo tu kitaifa bali hata kikanda na kimataifa. Mlipuko wa Ebola ambao haujawahi kushuhudiwa *kabla* huko Afrika Magharibi, mnamo 2014 na janga la Dunia la UVIKO - 19 mnamo 2019 vilizua hali ya wasiwasi mkubwa ambao, kwa muda, ilionekana kukosa majibu yenye ufanisi kitaifa na kimataifa, na matokeo ya majanga haya yalijidhihirisha kwenye afya na ustawi wa binadamu, usalama wa chakula, na wa kiuchumi. Mwaka 2005-2006, wakati Dunia inakabiliwa na tishio la vimelea vya homa ya mafua ya ndege ya *H5N1*, nchi nyingi za Afrika zilianzisha kamati za sekta mbalimbali ili kusaidia kukabiliana na tishio hilo.Wakati tishio hilo lilipodhibitiwa duniani kote, ufadhili mahususi ambao ulisaidia miundo hii, kufanya kazi, ulipungua au kutoweka kabisa na kamati hizo zikavunjwa. Hata hivyo, inategemewa kuwa, miundo iliyoundwa kukabiliana na Ebola na UVIKO - 19 kimataifa na kitaifa itaimarishwa na kuwa endelevu.

Uzoefu wa matukio ya hivi karibuni ya mlipuko, haswa wa homa ya mafua ya ndege, umechochea ongezeko la utambuzi wa umuhimu wa juhudi zinazoendelea za sekta nyingi kushughulikia matishio ya majanga. Dhana wa Afya Moja imeidhinishwa na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Kimataifa la Programu ya Mazingira (UNEP). Ushirikiano huu una lengo la kuboresha uzuiaji, utambuzi na kukabiliana na matishio ya magonjwa yanayoweza kujitokeza. Hata hivyo, maswali muhimu bado yanasalia kuhusu jinsi ya kuweka taasisi thabiti na kuiwezesha mbinu hii kufanya kazi katika nchi mbalimbali. Takriban asilimia 75 ya magonjwa yote yanayoibuka na kujirudia yanayoathiri wanadamu mwanzoni mwa Karne ya 21 yametokana na wanyamapori.

VVU/UKIMWI, Ugonjwa Mkali wa Kupumua na mafua ya ndege hutukumbusha wazi ni jinsi gani dunia iliyounganika inavyoweza kuwa hatarini kutokana na athari za magonjwa yanayoibuka sehemu yoyote duniani. Kasi ambayo magonjwa haya yanaweza kutokea na kuenea inaleta wasiwasi mkubwa wa afya ya jamii, kiuchumi na kimaendeleo kwa ujumla. Magonjwa haya pia yanasababisha haja ya kuanzisha uwezo mpana wa kutambua magonjwa, kuzuia, na kukabiliana kitaifa na kimataifa hasa katika maeneo yale yenye jiografia inayofanana ambapo kuna uwezekano wa kutokea matishio ya magonjwa. Kwa kutambua mahitaji yaliyoelezwa hapo juu, Mpango Mkakati huu unaainisha hapa chini, matishio muhimu zaidi ya kiafya yanayoelekea kujitokeza ambayo uwezo wa kutosha wa kutambua, kuzuia na kukabiliana nayo ni lazima uanzishwe.

### 1.5.1 Magonjwa ya Zuonotiki

Tanzania imepitisha magonjwa ya kipaumbele sita ya zuonotiki tangu 2016 wakati orodha ya vipaumbele vya pamoja ilianishwa kutokana na uchambuzi wa kimfumo wa vigezo vilivyopimwa na wawakilishi kutoka sekta tofauti. Vigezo hivyo vilikuja na magonjwa ya zuonotiki yaliyopewa kipaumbele ambayo ni pamoja na Kichaa cha mbwa, Homa ya Bonde la Ufa na homa nyingine za virusi vinavyosababisha magonjwa ya kutokwa na damu (*Marburg na Ebola*), mafua ya zuonotiki , Kimeta, malale (*Trypanosomiasis ya Kiafrika*) na Bruselosisi *(Brucellosis).* Hata hivyo, katika mlipuko wa UVIKO - 19 ambao uliibuka ulimwenguni mnamo 2019, ni dhahiri kwamba unapaswa kujumuishwa kama moja ya magonjwa ya kipaumbele ya zuonotiki. Kimataifa inajulikana na imethibitishwa kuwa asilimia 60-80 ya vimelea vya magonjwa ya binadamu, ikiwa ni pamoja na vile vinavyohusika na magonjwa ya milipuko yanayoibuka na kujirudia vina vyanzo mbalimbali, vingi vikitoka kwa wanyama.Uchunguzi umebaini kuwa zaidi ya asilimia 60 ya magonjwa ya kuambukiza yanayoibuka na kujirudia kwa wanadamu kiasili ni ya zuonotiki ; ambapo asilimia 72 vyanzo vyake ni wanyamapori.

Kwa hiyo, hii ina maana kwamba, aina yoyote ya mwingiliano wa karibu kati ya binadamu, mifugo na wanyamapori inaweza kusababisha athari kubwa ya mienendo ya magonjwa kwa wanadamu. Tanzaniani ya nne *kuwa na* viumbe hai ikitanguliwa na Brazili, Indonesia, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, hii ina maana kwamba, wigo wa hatari za wanyamapori kuwa chanzo cha maambukizi ya magonjwa kwa binadamu ni mkubwa, hasa katika maeneo ambayo kuna mwingiliano.

Hali ya ushirikiano kati ya binadamu na mifumo ya ikolojia ya wanyamapori na uvamizi wa mifumo hiyo unaoongeza ukataji miti ni ushahidi wa wazi wa uwezekano wa kuvuka kwa vimelea vya magonjwa kati ya wanyamapori, mifugo na binadamu.

Nchini Tanzania, imeonekana pia kwamba magonjwa ya homa, yanayosababishwa na magonjwa ya zuonotiki kama leptospirosisi, bruselosisi na *Q-fever*, mara nyingi yametambuliwa vibaya kama ugonjwa wa malaria.Utambuzi potofu unaotokana na ujuzi duni wa kiufundi wa wataalamu wa afya na uwezo mdogo wa mifumo ya afya mara nyingi umesababisha kutolewa kwa tiba isiyo sahihi na hivyo kusababisha wagonjwa kuugua kwa muda mrefu, ugonjwa kuwa tatizo kubwa pamoja na matumizi yasiyofaa ya dawa za malaria. Tanzania inakabiliwa na aina mbalimbali za matishio ya kiafya na madhara makubwa yanayotokana na magonjwa kadhaa ya zuonotiki , huku baadhi yao yakiwa yamepata uangalizi mdogo au kutopewa umuhimu unaostahili. Hii pia inaonesha kwamba, juhudi zilizowekwa kulinda afya ya binadamu zinapaswa kushughulikia hatari zinazohusishwa na aina mbalimbali za magonjwa ya zuonosia .

### 1.5.2 Usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (AMR)

Dawa dhidi ya vimelea vya magonjwa zina jukumu muhimu katika kupambana na magonjwa ya kuambukiza kwa binadamu na mifugo.Kuanzishwa kwa matumizi ya dawa ya penisilini katika karne ya 20 kulisababisha kupungua kwa kasi ya magonjwa na vifo kutokana na magonjwa ya kuambukiza yanayosababishwa na bakteria. Kinyume chake, tiba hiyo iliyoonekana ya muujiza iliyotolewa kwa antimikrobiamaambukizi ya kawaida ya bakteria ilishindwa kufanya kazi kutokana na bakteria hao kuwa sugu dhidi ya dawa hiyo (antimikrobia).

Usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (kama inavyofafanuliwa na WHO) ni dawa kushindwa kuviua vimelea vya magonjwa antimikrobia kama ilivyokuwa hapo

awali kwa matibabu ya maambukizi yanayosababishwa navyo. Usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa ni tatizo linalojitokeza la afya ya jamii duniani kote. Ingawa kuna data chache kuhusu usugu wa vimelea vya magonjwa antimikrobia nchini Tanzania, hata katika miaka ya 1990, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa katika matumizi ya kawaida, kama vile *ampicillin*, *tetracycline, chloroquine, na trimethoprim-sulfamethoxazole* ulikuwa umedhihirika.

Kupitia utaratibu wa uchaguzi wa matibabu ya magonjwa wa kawaida kwa kutumia antimikrobia, vimelea vya magonjwa polepole hukabiliana nayo na hatua kwa hatua huhitajika kiwango zaidi cha dawa hiyo mpaka inakuwa sugu kabisa kwa matumizi antimikrobia ambayo awali ilikuwa na ufanisi mkubwa. Tatizo hili limekuwa likijitokeza kwa miongo 5 iliyopita na linahatarisha uwezo wetu wa kuhudumia wagonjwa katika mifumo ya huduma za afya na hivyo, kusababisha milipuko ya magonjwa ambayo awali yalitibika kwa sababu ya usugu wa vimelea..Tatizo la AMR pia linahatarisha uwezo wetu wa kuendeleza usafirishaji wa chakula na kudumisha maendeleo ya taifa. Ikizingatiwa kuwa Usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa ni tatizo kubwa la afya ya jamii, antimikrobia. AMR inachukuliwa kuwa tatizo changamano la kiafya kutokana na sababu zake kuwa changamano, na suluhisho lake ni changamano. Hata hivyo, mjadala kuhusu matumizi ya antimikrobia katika kilimo inasalia kuwa mjadala mgumu kutokana na uhusiano wake na masuala mengine ya kisayansi, kisiasa na kiuchumi. Licha ya kutengenezwa kwa dawa mpya kuchukua nafasi ya zile sugu, AMR inaenea kwa kasi zaidi kuliko jitihada za uanzishwaji wa michanganyiko mipya katika matumizi ya kimatibabu, na hivyo kusababisha wasiwasi katika afya ya jamii. Jambo la kusikitisha zaidi kuhusu visababishi vya AMR ni pale binadamu anapotumia bidhaa za wanyama na mimea ambazo zimechafuliwa na antimikrobia ama kwa makusudi au kutokujua, kupitia matibabu, malisho au uchafuzi wa mazingira.

Matumizi kupita kiasi na matumizi mabaya ya antimikrobia huwezeshwa katika sehemu nyingi kutokana na upatikanaji wake kwenye kaunta za maduka bila agizo la daktari, lakini hata pale ambapo sivyo, mazoea ya kuagiza yanatofautiana sana kati ya nchi na nchi. Masuala kama haya yanafanywa kuwa mabaya zaidi na idadi kubwa ya dawa ghushi na za viwango vya chini vya antimikrobia zinazoenea katika masoko ya dawa katika baadhi ya maeneo. Katika baadhi ya maeneo barani Afrika dawa za kuua vijidudu huuzwa mitaani na katika masoko ya wazi na hivyo kuendeleza tatizo la AMR.

Matumizi ya antimikrobia katika kilimo yanaelezwa mara kwa mara kuwa chanzo kikuu cha tatizo la kiafya la magonjwa sugu katika dawa za binadamu. Kuku, mayai, nyama na bidhaa za maziwa tunazotumia mara nyingi huwa na dozi ndogo za antimikrobia ambazo zinaweza kusababisha usugu kwa wanadamu. Hii ni hali ya kuogofya sana kwani wengi wetu hutumia bidhaa hizi za wanyama tukiwa na ufahamu mdogo au bila kujua kabisa madhara yake kiafya. Ni dhahiri kwamba wafugaji hawawezi kufuata sheria au kanuni zinazowalazimisha kutupa mazao ya mifugo yasiyofaa kwa sababu yanaathiri maisha yao ya kiuchumi.

Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali ya Tanzania imepitisha Ajenda ya Bunge la 68 la Afya Duniani la Mei 2015, ambalo lilipitisha mpango kazi wa kimataifa kuhusu usugu wa vimelea vya magonjwa na kuzitaka Nchi Wanachama kuandaa Mipango ya Kitaifa (*National Action Plan - NAP*) ya AMR kwa kutumia "Mbinu ya Afya Moja" kama njia ya kushughulikia changamoto hii na masuala mengine magumu. Mpango wa Kitaifa wa utekelezaji uliainisha malengo makuu ya kimkakati, afua, na shughuli za kupunguza kasi ya ukuaji na kuenea kwa AMR na kuboresha *afya* ya mgonjwa. Malengo ya NAP ni: Kuboresha ufahamu na uelewa wa usugu wa vimelea

vya magonjwa kupitia mawasiliano, elimu na mafunzo yenye ufanisi; Kuimarisha msingi wa maarifa na ushahidi kupitia ufuatiliaji na utafiti; kupunguza matukio ya maambukizi kwa njia ya usafi wa mazingira, usafi wa mtu binafsi na hatua za kuzuia maambukizi; Kuboresha matumizi ya dawa za antimikrobia katika afya ya binadamu na wanyama; kuendeleza masuala ya kiuchumi kwa uwekezaji endelevu unaozingatia mahitaji ya nchi zote na kuongeza uwekezaji katika dawa mpya, zana za uchunguzi, chanjo na afua zingine.

### 1.5.3 Matishio ya Usalama wa Afya na Ulinzi wa Kibiolojia

Usalama wa Afya maana yake ni hatua za usalama zilizowekwa ili kukinga au kuzuia watu wasidhurike kutokana na kuathiriwa na vimelea au sumu zinazoambukiza pasipo kukusudia (au kwa kifupi, kuzuia athari kwa watu kutokana na vimelea vya magonjwa). Usalama na ulinzi wa kibiolojia maana yake ni hatua za usalama zilizowekwa ili kuzuia upotevu, wizi, matumizi mabaya, ubadilishaji, au kutoa kwa makusudi vimelea na sumu zinazoambukiza wanyama au binadamu (au kwa kifupi, kuzuia vimelea visipitishwe mikononi mwa watu wasio waaminifu).Kwa upande mwingine, Udhibiti wa Vihatarishi unamaanisha mfumo mzima na michakato iliyowekwa ili kudhibiti hatari za Usalama wa Uhai na Mazingira zinazohusiana na utunzaji au uhifadhi na utupaji wa vimelea vya kuambukiza au sumu katika huduma za afya ya binadamu, wanyama na mazingira.

Mahitaji ya kutekeleza Udhibiti wa Vihatarishi yanaongezeka kutokana na kuongezeka kwa hatari za usalama na ulinzi wa viumbe zinazohusiana na matukio ya magonjwa yanayoibuka na kujirudia, yanayoathiri wanadamu, wanyama na mimea na kusababisha athari kubwa kiafya na kiuchumi nchini. Vihatarishi (vya kibiolojia) vinavyohusishwa ni milipuko ya Homa ya Bonde la Ufa katika Afrika Mashariki (2006-2007), sumu kuvu (2016); na janga la kimataifa la UVIKO - 19 (2019) ni mifano michache tu ya vihatarishi vinavyoathiri wanadamu, wanyama na mimea, ambavyo vinaweza kujumuisha matatizo changamano ya kiafya.

Zaidi ya hayo, kuongezeka kwa mwingiliano wa binadamu na wanyama wa nyumbani, wanyamapori na mazingira kwa pamoja huongeza mzunguko wa changamoto hizo za kiafya na kiuchumi. Aidha, ongezeko la watu duniani hasa katika nchi zinazoendelea, shughuli za usafiri na usafirishaji, na ukuaji wa miji, linahusishwa na hatari za milipuko ya magonjwa, ugaidi wa kibiolojia na dharura nyingine za afya ambazo zinatishia maisha. Kwa hiyo, juhudi za pamoja za wataalamu wa sekta za afya ya binadamu, wanyama na mazingira pamoja na taratibu za uratibu wa sekta mbalimbali zilizopangwa vyema kupitia mbinu ya Afya Moja ni za umuhimu mkubwa na zinaweza kutoa suluhu kwa matatizo haya changamano. Hivyo, kujumuisha shughuli za Usalama wa Uhai na Usalama wa viumbe katika Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Afya Moja na kuratibu utekelezaji wake kupitia Sehemu ya Afya Moja, kutasaidia kuongeza kasi ya utekelezaji wa Usimamizi wa Vihatarishi na kuboresha usalama na ulinzi wa kibiolojia na wa nchi kwa ujumla.

### 1.5.4 Matishio ya Usalama wa Chakula

Mlipuko wa magonjwa katika mifugo siyo tu unaweka hatarini chanzo cha kawaida cha chakula, lakini pia unaweka hatarini maisha yao na uwezo wao wa kustahimili hali hiyo na kuathiri usalama wao kwa muda mrefu. Milipuko ya magonjwa ambayo hupunguza upatikanaji wa wanyama hai na mazao ya mifugo inaweza kupunguza mapato ya kaya, kudhoofisha mlo wa wanakaya, kudhoofisha hali ya lishe na kuongeza hatari

kwa afya, hasa kwa wanawake na watoto. Aidha, milipuko inaweza kudhoofisha upatikanaji wa soko kwa bidhaa hizo. Ukosefu wa usalama wa chakula kwa muda mrefu pia husababisha tabia hatarishi zinazohusiana na upatikanaji wa nyama, mfano hakuna mtu ambaye ana uhakika wa usalama wa chakula angefikiria kula mzoga. Madhara ya magonjwa ya wanyama yanaenea kwa wafanyakazi wanaofanya kazi za uzalishaji na uchakataji – kwa maao ya mifugo, kilimo, wasafirishaji, na wauzaji.

Dhana ya Afya Moja husaidia kutafuta njia za kupunguza hatari hizi na kusisitiza kutafuta riziki za maisha zinazostahimili. Magonjwa ya zuonotiki yana madhara makubwa kwa usalama na ulinzi wa chakula; hata hivyo, Tanzania haina wakala unaohusika na usalama wa chakula. Udhibiti wa usalama wa chakula una mfumo unaohusisha Wizara, idara na taasisi mbalimbali. Usalama wa chakula pia unahusishwa na AMR ambapo vyakula vya mifugo vinaweza kuwa na viwango vidogo vya antimikrobia na mazingira yanaweza kuwa na mabaki ya antimikrobia ambayo yanaweza kusababisha AMR. Kuna haja ya kutunga na kuimarisha sheria, kanuni, viwango na mifumo ya uratibu wa Usalama wa Chakula, ili kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika ipasavyo, kudhibiti uchafuzi wa kemikali, mionzi na mikrobiolojia kwa ufanisi.

### 1.5.5 Matishio ya Afya ya Mazingira

Afya ya mazingira inahusika na nyanja zote za mazingira asilia na yaliyojengwa yanayoathiri afya ya binadamu. Kwa upande mwingine, ulinzi wa mazingira unahusika na kulinda mazingira asilia kwa manufaa ya afya ya binadamu na mfumo wa ikolojia. Mazingira na mambo yanayohusiana nayo ni sehemu nyingine *ya* sababu *za* magonjwa mengi ya mlipuko katika mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea.

Nchini Tanzania, matatizo ya afya ya mazingira yanatokana na ongezeko la watu kwenye makazi, usafi duni wa mazingira, pamoja na ukosefu wa maji safi na salama na huduma dunikatika makazi. Licha ya hali mbaya ya afya ya mazingira, kuna changamoto za ufuatiliaji kwa wakati.
Idadi kubwa ya watu nchini Tanzania wanaishi katika umaskini na hawapati huduma za msingi kama vile chakula, maji safi na salama, vyoo na usafi wa mazingira na hivyo kusababisha uwezekano wa kuambukizwa magonjwa. Hivyo, kuna umuhimu wa kuwekeza zaidi katika afya ya mazingira na kuhakikisha kila Mtanzania anapata majisafi na salama, njia sahihi za kutupa taka na usafi wa mazingira unaostahili. Hii itasaidia sana kuzuia kuenea kwa magonjwa.

### 1.5.6 Matishio ya kiafya katika mabadiliko ya tabianchi

Tofauti ya hali ya hewa inahusishwa na usambaaji wa kijiografia na kualiana kwa vekta wanaohusika na magonjwa mbalimbali. Magonjwa katika mazingira yanayowakutanisha binadamu na wanyama (k.m., magonjwa ya zuonotiki , magonjwa yanayoenezwa na maji/chakula, magonjwa yanayoenezwa na wadudu) yanaendelea kuwa tishio kwa wanadamu na wanyama na ongeeko la maambukii na vifo. Magonjwa ya mlipuko yanayosababishwa na vekta kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ni pamoja na malaria, dengi, homa ya bonde la ufa, homa ya manjano na malale. Kwa mfano, homa ya bonde la ufa kwa kawaida huchochewa na mvua nyingi zinazonyesha kwa muda mrefu. Kwa upande mwingine, hali ya hewa ya joto, mzunguko wa mafuriko na ukame unachochea magonjwa yanayoenezwa na maji kama vile homa ya matumbo na kipindupindu. Kuenea kwa mlipuko wa kipindupindu kunaambatana na utabiri wa hali ya hewa nchini. Tafiti zinaonesha uhusiano mkubwa

kati ya hali ya joto na matukio ya kipindupindu nchini. Inatabiriwa kuwa kwa kila ongezeko la nyuzi joto 1 kuna ongezeko la hatari ya awali ya kipindupindu kwa asilimia 15 hadi 29. (Demographic Health Survey 2010 na 2015, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Dar es Salaam).

Licha ya kuwepo kwa uhusiano kati ya mabadiliko ya tabianchi na magonjwa yanayosababishwa na hali ya hewa nchini, kuna changamoto katika mfumo wa ufuatiliaji wa magonjwa hayo pamoja na kuwepo kwa mfumo wa usimamizi wa taarifa za afya. Uimarishaji wa Afya Moja unaweza kusaidia kutoa tahadhari kuhusu matukio ya ugonjwa na milipuko na hivyo kupanga mwitikio kwa wakati.

### 1.5.7 Matishio ya kiafya kutokana na majanga yanayoibuka na yanayojirudia

Mbali na vichocheo vya matishio ya  Magonjwa vilivyoorodheshwa hapo juu, Tanzania inakabiliwa na hatari nyingine nyingi za afya ya jamii kama vile magonjwa yatokanayo na chakula kwa mfano sumu kuvu, kipindupindu na kifua kikuu.Sumu kuvu ni mfano wa wazi wa hatari za kiafya ambazo zinaweza kuhusishwa na ulaji wa vyakula vyenye vimelea vya magonjwa  na sumu. Mojawapo ya njia za kawaida ambazo magonjwa ya mimea yanaweza kuathiri wanadamu ni kupitia utolewaji wa metaboliti zenye sumu kama vile mikotoksini kwa  bidhaa za mimea.

Ingawa Kuvu wanaozalisha mikotoksini huambukiza mimea lakini si wanadamu, sumu hizo mara nyingi huwa na athari mbaya kwa afya ya binadamu na wanyama. Aflatoksini ni mojawapo ya makundi ya kawaida na makubwa (aina = B1, B2, G1 na G2), ambayo hutolewa na baadhi ya aina za Kuvu (*Aspergillus*). Aflatoksini B1 ni mojawapo ya sumu kali zaidi za mikotoksini kwa sababu ni hatari kwa viwango vya juu na inaweza kusababisha kansa kwa wanadamu kwa kiwango cha chini na inaweza kusababisha kupungua kwa utendaji *kazi* wa ini, kutapika na maumivu ya tumbo. Vifo vya kila mwaka katika baadhi ya maeneo ya Afrika kutokana na athari za aflatoksini vimeripotiwa *na* kufikia 250,000. Aidha, kipindupindu ni hatari kwa afya ya binadamu nchini Tanzania, na hii ni kwa sababu ya milipuko ya mara kwa mara ambayo nchi imeshuhudia. Sababu kuu zinazohusishwa na mlipuko huo ni: mafuriko, ukosefu wa maji safi na salama ya kutosha; usafi duni; mazingira machafu na kiwango kidogo cha elimu/uelewa wa jamii kuhusu magonjwa na vihatarishi vyake.

Barani Afrika, magonjwa ya mazao yana madhara makubwa kwa ustawi wa jamii kwani yanaweza kuwa sababu ya umaskini uliokithiri unaohusishwa na ukosefu wa chakula na lishe. Ukaushaji hafifu na uhifadhi mbaya wa nafaka na  bidhaa nyingine za chakula  ndiyo sababu kuu  hatarishi ya usalama wa chakula  na kuwa na sumu hatari kwa wanadamu na wanyama. Kwa upande mwingine, mlipuko wa *E. coli 0157* wa 2011 huko Ulaya na ule wa Japani mnamo 1996 na nchini Kanada mwaka 2000 pia inaashiria uwezekano wa Tanzania kukumbwa na visa kama hivyo, ingawa hakuna uwezekano wa vipimo vya milipuko. Ripoti za kuwepo kwa *E. coli 0157* katika wanyama [*Lupindu, 2014*] na binadamu [*Erb na wenzake., 2018*] nchini Tanzania zinaonesha uwezekano huu, ambao unaweza kuhusishwa na  ulaji wa mboga na matunda yaliyochafuliwa na samadi au maji taka.

Nchini Tanzania, sekta ya madini ni shughuli ya kiuchumi inayokua ambayo imesababisha kuibuka kwa shughuli za uchimbaji mdogo  zisizodhibitiwa wala kusimamiwa. Shughuli hizi, wakati fulani zimekuwa zikihusishwa na uchafuzi mkubwa wa vyanzo vya maji na hata maeneo ya malisho ambao umeshuhudiwa katika baadhi

ya maeneo ya Tanzania, jambo ambalo linaweza kuleta hatari kubwa kwa afya ya binadamu na wanyama, ikiwamo rasilimali za majini. Vilevile, uchafuzi wa mazingira na taka za viwandani katika maeneo ya mijini pia huleta hatari kwa afya ya binadamu na mfumo wa ikolojia. Kwa hiyo, udhibiti wa magonjwa haya unahitaji mkabala wa sekta mbalimbali unaojumuisha sekta ya afya ya binadamu, wanyama na mazingira, pamoja na maji, uhandisi/ujenzi; na elimu.

## 1.6 Mbinu ya Afya Moja

Mbinu ya Afya Moja inatambuliwa na Shirika la Afya Duniani, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Umoja wa Mataifa la Programu ya Mazingira na Ajenda ya Usalama wa Afya Duniani (GHSA) kama mkakati wa kukuza juhudi za pamoja za taalumba mbalimbali, kufanya kazi kuanzia ngazi ya chini, kitaifa na kimataifa, ili kuboresha afya ya jamii, wanyama na mazingira. Changamoto za kipaumbele za afya ya jamii ambazo hushughulikiwa kwa kutumia mbinu ya Afya Moja ni pamoja na: magonjwa ya zuonotiki; usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa; usalama wa chakula la lishe; usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi vya magonjwa; uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi na matishio ya afya ya jamii yanayoibuka.

Mbinu ya Afya Moja ni mkakati ambao nchi wanachama wa Shirika la Afya Duniani zinapaswa kuzingatia na kuwa sehemu ya utekelezaji wa Kanuni za Afya za Kimataifa (IHR) 2005 zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kuboresha ubainishaji na kutoa taarifa za dharura za afya ya jamii ulimwenguni. IHR 2005 zinatoa mfumo elekezi wa ufuatiliaji, utayari na kukabili matukio ya afya ya jamii yanayohusu mataifa, ikijumuisha zuonosia ndani ya mwamvuli wa mpango wa GHSA. Mwaka wa 2006, Kamati ya Kikanda ya Afrika (chombo cha uamuzi cha Shirika kuhusu sera ya afya katika Kanda ya Afrika) kupitia Azimio AFR/RC56/R2 ilitoa wito wa utekelezaji wa IHR (2005) katika muktadha wa Ufuatiliaji na Ukabilianaji jumuishi wa Magonjwa (IDSR) barani Afrika.

## 1.7 Mbinu ya Mfumo wa Afya Moja Tanzania

Tanzania ikiwa mjumbe wa WHO na Kamati ya Kikanda ya Afrika, iliona ni muhimu kuzingatia Azimio la IHR (2005) na kuridhia makubaliano ya kimataifa. Azimio la Tanzania la kufuata mfumo wa Afya Moja lilikuja baada ya mlipuko wa Homa ya Bonde la Ufa (RVF) mwaka 2007. Madhara makubwa ya RVF kwa afya ya binadamu na wanyama, pamoja na uchumi, yalichochea Ofisi ya Waziri Mkuu (OWM) kuratibu ukabilianaji ambao ulitekelezwa kwa pamoja na Wizara yenye dhamana ya Afya ya binadamu na Wizara yenye dhamana ya afya ya Mifugo. Kuimarishwa kwa mawasiliano ya kisekta wakati wa mlipuko huo kuliwezesha jitihada za kukabnili magonjwa kufanyika kwa ufanisi.

Baada ya mlipuko wa RVF, mamlaka za Tanzania zilifanya kazi ya kuweka mfumo wa Afya Moja kama taasisi ili kuwezesha uratibu wa utekelezaji wa afua unaofaa ambao unaweza kuzuia milipuko ya siku zijazo au kupunguza madhara ya magonjwa kwa wanadamu na wanyama. Uamuzi huu ulipelekea kuanzishwa kwa Dawati la Uratibu wa Afya Moja na kuandaa Mpango Mkakati wa Afya Moja wa 2015-2020 ambao ulilenga kufikia malengo yafuatayo:

i. Kuongeza uelewa juu ya Afya Moja kwa wataalamu, watunga sera na jamii;

ii. Kuimarisha mipango ya kujitayarisha na kuboresha uwezo wa kukabiliana na mlipuko wa magonjwa wa zuonotiki katika ngazi zote (jamii, Wilaya, Mkoa na Taifa);;
iii. Kuboresha afya ya binadamu, wanyama na mazingira kupitia utafiti unaozingatia uthibitisho;
iv. Kuweka mifumo ya kiutendaji yenye ubora iliyounganishwa ya afya ya binadamu na wanyama, katika ngazi zote, ili kupunguza athari za magonjwa ya zuonotiki ; na
v. Kuimarisha mifumo ya kitaasisi ili kusaidia utekelezaji wa Afya Moja.

Dawati la Uratibu wa Afya Moja lilipewa jukumu la kuratibu shughuli za vikosi kazi vya kitaalamu (Mafunzo, Utetezi na Mawasiliano; Kujuiandaa na Kukabiliana; Utafiti na Maendeleo; Ufuatiliaji) na Kamati ya Kitaalamu ya Kitaifa ya Sekta mbalimbali ya Afya inayojumuisha wakurugenzi kutoka Wizara, Taasisi na Sekta ongozi za Afya Moja (afya ya binadamu, afya ya wanyama (mifugo na wanyamapori) na mazingira) ili kuwezesha utekelezaji wa afua mbalimbali na ubadiishanaji wa taarifa katika sekta zote za afya ili kupunguza milipuko na kuokoa maisha.

## 1.8 Uratibu wa Afya Moja

Shughuli za Afya Moja huratibiwa na Sehemu ya Afya Moja, chini ya Idara ya Uratibu wa Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, ili kuwezesha ushirikiano na mawasiliano kati ya sekta na taaluma mbalimbali baina ya wadau wa afya moja , kwa ajili ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yanayoenea kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu katika mazingira, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, usalama wa chakula na lishe, usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi vya magonjwa. Sehemu ya Afya Moja inaratibu uhusiano na mawasiliano baina ya sekta na taaluma mbalimbali, katika ufuatiliaji, uzuiaji, udhibiti na upunguzaji wa madhara ya milipuko ya magonjwa yanayoibuka na yanayojirudia na matishio mengine ya afya ya jamii. Pia inaratibu majukumu ya wadau mbalimbali wa Afya Moja kama vile Wizara, sekta binafsi, AZISE za Kimataifa na za ndani, Taasisi za Kitaaluma na Utafiti, Asasi za kijamii, kidini na vyombo vya habari.

Muundo wa uratibu wa Afya Moja unafungamana na Mfumo wa Usimamizi wa Maafa katika ngazi zote. Sehemu ya Afya Moja chini ya Idara ya Uratibu wa Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, imepewa mamlaka ya kuratibu shughuli za Afya Moja au programu zinazotekelezwa na Wizara za kisekta, Taasisi, Kamati za Afya Moja za Kitaalamu na Vikosi Kazi vya kitaalamu vya aina Mbalimbali. Kuna Kamati za Afya Moja za Kitaalamu zinazoundwa na Waalamu wa sekta mbalimbali katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa ambazo zinasaidia sehemu ya Afya Moja kutekeleza majukumu yake katika ngazi husika. Vikosi Kazi vya kitaalamu katika ngazi ya taifa vinavyoundwa na wataalam kutoka Sekta mbalimbali vina jukumu la kushughulikia maeneo sita ya kimkakati ambayo ni:
(i) Mafunzo na Elimu (ii) Uhamasishaji, Utetezi na Mawasiliano, (iii) Kujianda na kukabiliana (iv) Utafiti na Maendeleo (v) Ufuatiliaji, uzuiaji na udhibiti na (vi) Uratibu.

Sehemu ya Afya Moja hutumika kama sekretarieti ya Kamati ya Wataalam ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa kwa masuala yote yanayohusiana na matishio ya majanga yanayohatarisha afya ya jamiina kutoa mwongozo na kukusanya rasilimali kwa ajili ya kuzuia au kukabiliana na matishio ya afya.

## 2. UCHAMBUZI WA HALI ILIYOPO

Sura hii inaelezea tathmini ya utaratibu *wa* utendaji wa shughuli za Afya Moja. Inatathmini uwezo wa sasa na *wa baadaye*, udhaifu, fursa na changamoto, na pia uwezo wa ndani na nje unaoweza kuathiri utendaji na uchaguzi wa mikakati.

### 2.1 Utekelezaji wa Kanuni za Afya za Kimataifa (IHR (2005))

Nchi Wanachama wa Shirika la Afya Duniani hutumia IHR (2005) kusimamia ufuatiliaji wa dharura za afya ya jamii zinazoshughulikiwa kimataifa. Miongozo hii ilitungwa mwaka wa 2005 na ilianza kutumika tarehe 15 Juni 2007 na inatumika kisheria. Mwaka 2006, Kamati ya Kanda ya Afrika kupitia Azimio AFR/RC56/R2 ilitoa wito wa kutekelezwa kwa IHR (2005) katika muktadha wa ufuatiliaji na ukabilianaji jumuishi wa Magonjwa (IDSR).

Utekelezaji wenye mafanikio wa IHR 2005 unahitaji utimilifu wa uwezo katika maeneo 8 ya msingi ikiwa ni pamoja na sheria, sera na uratibu, ufuatiliaji, utayari, ukabilianaji, mawasiliano kuhusu hatari, maabara na rasilimali watu kwa ngazi zote ikiwa ni maeneo ya mipakani, pamoja na majanga yanayoweza kutokea (matukio ya zoonotic). Uimarishaji wa maeneo ya msingi ya IHR katika matukio ya zuonotiki kulingana na viwango vya uwezo ni kama ifuatavyo:

**Kiwango cha 1 cha Uwezo: Msingi**.

a. Kuwepo kwa uratibu ndani ya mamlaka ya serikali inayowajibika kuhusu utambuzi na kukabiliana na matukio ya zuonotiki.
b. Kuwepo kwa orodha ya magonjwa ya zuonotiki ya kipaumbele na ufafanuzi wa matukio husika.
c. Kuwepo kwa orodha inayohuishwa mara kwa mara ya wataalamu wanaoweza kushughulikia matukio ya zuonotiki.

**Kiwango cha 2 cha Uwezo: Nyaraka na michakato**

a. Kuwepo kwa Sera ya kitaifa, mkakati au mpango wa ufuatiliaji na kukabiliana na matukio ya zuonotiki
b. Kuwepo kwa mratibu anayehusika na afya ya wanyama (pamoja na wanyamapori) aliyeteuliwa kwa ajili ya uratibu wa utekelezaji wa IHR 2005 kwa kushirikiana na Wizara ya Afya .
c. Ukusanyaji na ulinganishajiwa data za magonjwa ya zuonotiki kwa mpangilio maalumu na kwa wakati .
d. Upatikanaji wa maabara zenye uwezo, kitaifa au kimataifa (kupitia taratibu zilizowekwa) ili kuthibitisha matukio ya kipaumbele ya /magonjwa ya zuonotiki .
e. Kuanzishwa kwa utaratibu wa kukabiliana na milipuko ya magonjwa ya zuonotiki kwa sekta za afya ya binadamu na wanyama.

**Kiwango cha 3 cha Uwezo: Matokeo**

a. Kuanzishwa kwa taratibu za kiutendaji za ushirikiano wa sekta mbalimbali zinazojumuisha vitengo na maabara za uchunguzi wa afya ya wanyama na binadamu..
b. Utekelezaji wa ufuatiliaji wa magonjwa ya zuonotiki unaohusisha jamii.

c. Ubadilishanaji wa taarifa kwa wakati na kwa utaratibu kati ya vitengo vya uchunguzi wa wanyama, uchunguzi wa afya ya binadamu na sekta nyingine husika kuhusu hatari zinazoweza kutokea za magonjwa na matukio ya dharura ya zuonotiki
d. Kukabili kwa wakati kwa zaidi ya asilimia 80 ya matukio ya zuonotiki ya kitaifa na kimataifa.

### Kiwango cha 4 cha Uwezo: Mafanikio ya ziada

Kushirikishana uzoefu na matokeo ya tafiti za nchi zinazohusiana na hatari za zuonotiki na matukio yenye uwezekano wa kutokea ya kitaifa na kimataifa na jumuiya ya kimataifa.

## 2.2 Tathmini na Uboreshaji wa Mifumo ya Afya

Tathmini ya Pamoja ya Nje (WHO – JEE) ni mfumo unaotumiwa kutathmini uwezo wa nchi katika kuzuia, kutambua na kukabiliana na matishio ya afya ya jamii.Tanzania ni nchi ya kwanza kufanya tathmini ya JEE mwaka 2016 ambapo uwezo wa nchi katika maeneo 19 ya kitaalamu ulipimwa. Matokeo yalionesha kuwa ingawa kumekuwa na maendeleo makubwa, lakini upungufu bado upo katika uwezo wa kuzuia, kutambua na kushughulikia dharura za afya ya jamii.

Kutokana na tathmini ya JEE mwaka 2015 NAPHS iliandaliwa mwaka 2017-2021 ili kushughulikia upungufu ulioainishwa. Tanzania ilijiunga na mpango wa GHSA unaolenga kuchangia katika kushughulikia masuala ya usalama wa afya katika ngazi ya kimataifa pamoja na kuharakisha utekelezaji wa IHR nchini., OIE imeunda Njia ya Utendaji wa Huduma za Mifugo (PVS), ambayo inajumuisha zana tofauti kusaidia nchi kutathmini na kushughulikia udhaifu wa Huduma za Mifugo ili kuwa na uboreshaji endelevu wa Huduma za Kitaifa za Mifugo kwa viwango vya OIE.Tanzania ilifanya uchambuzi wa upungufu wa OIE -PVS mwaka 2009 na ufuatiliaji wa tathmini ya PVS mwaka 2016 ambao ulibaini upungufu katika utoaji wa huduma za mifugo. Mnamo mwaka wa 2019 warsha ya kuunganisha IHR-PVS ilifanyika ili kuchambua na kuboresha ushirikiano kati ya sekta za afya katika kuzuia, kutambua na kukabiliana na magonjwa ya zuonotiki na matukio mengine ya afya katika mazingira yanayowakutanisha binadamu na wanyama.

## 2.3 Mfumo wa Udhibiti

Kuna sheria na kanuni mbalimbali zinazoongoza utekeleaji wa Mbinu ya Afya Moja nchini ambazo ni:
a. **Sera ya Taifa ya Afya, 2007:** Sera ya Taifa ya Afya inatoa mwelekeo wa uboreshaji na uendelevu wa hali ya afya ya watu wote, kwa kupunguza ulemavu, maradhi na vifo, kuboresha hali ya lishe na kuongeza umri wa kuishi.
b. **Sera ya Taifa ya Mifugo ya 2006:** Sera hiyo inatoa mwongozo wa udhibiti wa magonjwa ya zuonotiki kwa lengo la kulinda afya ya jamii Tanzania.
c. **Mpango Kazi wa Kitaifa wa Usalama wa Afya wa 2017-2021:** Huu ni Mpango Mkuu ambao unaelezea hatua na afua zinazopaswa kutekelezwa kwa kuzingatia IHR.
d. **Mpango Kazi wa Kitaifa Kuhusu Usugu wa Vimelea vya Magonjwa Dhidi ya Dawa wa 2022 - 2027:**
Mpango Kazi wa Kitaifa unaoshughulikia hatua zinazohitajika kuchukuliwa ili kukabiliana na AMR nchini. Inapaswa kuongeza uelewa wa AMR na kuhamasisha mabadiliko ya tabia kupitia programu za mawasiliano ya umma zinazolenga afya ya binadamu, wanyama na mimea. Kujumuishwa kwa matumizi ya mawakala wa

antimikrobia na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa katika mitaala ya shule kutakuza zaidi uelewa na ufahamu kuanzia umri mdogo.

e. **Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa 2022:**
Mpango unakusudia kufafanua vipengele vyote vya shughuli za dharura katika ngazi zote, kama vilekupanga, kujiandaa na kukabili matukio ya dharura mbalimbali.

f. **Mpango Mkakati wa sekta ya afya (2021 -2027)**: Mkakati huo unatambua kuwa mafanikio katika sekta ya afya hayawezi kufikiwa na kudumu bila kushirikisha Wizara kuu, Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara nyingine za kisekta zikiwemo, Wizara za maji, kilimo, uvuvi na mifugo, miundombinu ya TEHAMA na nyingine ambazo zinahusika kwa namna moja au nyingine katika sekta ya afya. Ushirikiano wa sekta mbalimbali utaimarishwa chini ya uongozi wa OWM ili kuhakikisha kuwa mbinu ya afya katika sera zote inatekelezwa ipasavyo.

g. **Mkakati wa Kitaifa wa Afya wa Kielektroniki 2013**: Mkakati huo unatambua uwezo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) unaoweza kubadilisha utoaji wa huduma ya afya kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa na kusaidia shughuli za huduma ya afya, usimamizi, na kufanya uamuzi.

h. **Sheria ya Magonjwa ya Wanyama namba 17, 2003:** Kutoa uthibitisho, uchunguzi wa mlipuko wa magonjwa ya wanyama, udhibiti, taarifa na fidia.

i. **Sheria ya Veterinari Na 16, 2003:** Sheria hii inatoa masharti ya usajili wa madaktari wa mifugo, uandikishaji au uorodheshaji wa Wataalamu na Wasaidizi wa Wataalamu, kwa ajili ya kuanzishwa kwa Baraza la Mifugo na kwa masuala yanayohusiana na hayo.

j. **Sheria ya Afya ya Jamii Na. 1, 2009**: -Sheria hii inatoa utaratibu wa uendelezaji wa uhifadhi na udumishaji wa afya ya jamii kwa nia ya kuhakikisha utoaji wa huduma kamili na endelevu za afya ya jamii kwa ujumla. Inatumika kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ikiwa ni pamoja na zuonosia, Sheria inatoa mwongozo wa namna ya kutoa taarifa ya kuzuka kwa tukio na uchunguzi wake.

k. **Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na.6, 2022**: Sheria hii inaelekeza uanzishwaji wa mfumo wa usimamizi wa maafa, usimamizi wa hatari za maafa, utaratibu wa uratibu wa kuzuia maafa, kupunguza, kujiandaa, kukabiliana na maafa, uanzishaji na usimamizi wa mfuko wa usimamizi wa maafa na masuala mengine yanayohusiana nayo.

l. **Sheria ya Nishati ya Atomiki, Namba 7 ya 2003:** Sheria hii inaanzisha Tume ya Nishati ya Atomiki Tanzania ambayo ni chombo cha kitaifa cha udhibiti kinachohusika na masuala ya nishati ya atomiki nchini.

m. **Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20, 2004**: Sheria inaelezea mfumo wa kitaasisi kwa usimamizi endelevu wa mazingira; kuainisha kanuni za usimamizi, athari na tathmini ya hatari, kuzuia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira, usimamizi wa taka na viwango vya ubora wa mazingira.

n. **Sheria ya Uvuvi namba 22 ya 2003:** Sheria inaweka masharti ya maendeleo endelevu, ulinzi, uhifadhi, ufugaji wa samaki, udhibiti wa samaki, mazao ya samaki, mimea ya majini na mazao yake na mambo yanayohusiana nayo.

## 2.4 Majukumu na Kazi za Sehemu ya Afya Moja

Mamlaka ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya kuratibu Maandalizi na Usimamizi wa Matukio ya Maafa yametolewa katika Notisi ya ugawaji wa Kazi za  Wizara, rejea Tangazo la Serikali Na. 385 ya tarehe 7 Mei, 2021. Majukumu ya Sehemu ya Afya Moja ni pamoja na:

i. Kuratibu na kutoa mwongozo wa jumla juu ya ushirikiano baina ya  sekta kwenye shughuli za Afya Moja na magonjwa yasiyo ya kuambukiza;
ii. Kuratibu maandalizi na mapitio ya sera, sheria na kanuni kuhusu Afya Moja

iii. Kufuatilia masuala yote yanayohusiana na milipuko ya magonjwa ya binadamu na wanyama; uvamizi wa wadudu; AMR; Usalama wa Chakula na Lishe; aflatoksini na kushauri ipasavyo;
iv. Kuratibu shughuli za Afya Moja katika Wizara, idara na wakala  husika ikijumuisha sekta binafsi katika utekelezaji wa mikakati, mipango na miongozo ya Afya Moja;
v. Kusaidia kutafuta rasilimali za kutekeleza programu, miradi na shughuli za Afya Moja

vi. Kuhamasisha ushirikishanaji wa data, taarifa, nyenzo na rasilimali nyingine za Afya Moja;

vii. Kuratibu mifumo ya  kukabiliana na  maafa kwa wakati ikijumuisha utumaji wa timu za  utayari katika hali ya matukio yasiyo ya kawaida, na kufanya tathmini wakati na baada ya tukio;

viii. Kuratibu shughuli za maafa yanayovuka mipaka kuanzia kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ya afya ya binadamu na wanyama na mlipuko wa wadudu;

ix. Kuratibu Wizara na taasisi ongozi na washirika katikakutekeleza taratibu za uendeshaji  *wa* masuala yanayohusiana na kuzuia, kutambua na kukabiliana na dharura za afya ya jamii;
x. Kuratibu ushirikiano na Zanzibar katika kuzuia, kutambua na kukabiliana na dharura za afya ya jamii
Xi. Kuratibu jamii katika kuzuia na kudhibiti dharura za afya ya jamii kupitia kamati za maafa za mikoa, wilaya, kata na vijiji.

## 2.5  Mfumo wa Afya ya Binadamu, Wanyama Na Mazingira Tanzania

Sehemu hii inaelezea kwa kifupi miundo ya kitaifa ya Wizara muhimu zinazofanya shughuli za Afya Moja kutoka ngazi ya jamii hadi Kitaifa.

### 2.5.1   Wizara ya Afya

Wizara ya Afya  (MoH) inatekeleza ajenda ya Afya Moja kupitia sera ya Afya ya Taifa (2017) kwa ushirikiano wa taaluma za sayansi ya afya pamoja na taasisi zinazofanya

kazi ndani, kitaifa na kimataifa ili kufikia afya bora kwa watu, wanyama wa nyumbani, wanyamapori, mimea na mazingira. Wizara imeandaa mpango wa kujiandaa na kukabiliana na dharura, uanzishwaji wa kituo cha kuratibu operesheni za dharura ambacho kinaunganishwa na Kituo cha Taifa cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura kwa ajili ya uratibu wa kukabiliana na maafa kitaifa , utekelezaji wa mfumo wa Shirika la Afya Duniani wa Ufuatiliaji na Ukabilianaji Jumuishi wa Magonjwa yaani IDSR kama njia ya ufuatiliaji wa magonjwa kutoka ngazi ya jamii hadi Taifa. Miongozo ya IDSR ni kama njia ya ufuatiliaji wa magonjwa kutoka ngazi ya jamii hadi Taifa. Miongozo ya IDSR ni pamoja na itifaki za ufuatiliaji na ukabilianaji wa magonjwa 33 yanayoweza kutambuliwa na kutolewa taarifa kwa harakaau kila wiki kwa lengo la kutambua magonjwa kwa wakati, uchunguzi na hatimaye kukabili kwa haraka.

Wizara imeanzisha Mpango wa Mafunzo ya ufuatiliaji wa Magonjwa na Maabara Tanzania (FELTP) kwa wahudumu wa afya ya binadamu na wanyama katika Wilaya na vituo vya kutolea huduma za afya ili kuimarisha uwezo wa *kutambua* magonjwa. Mipango mingine ya wizara ya kuimarisha mbinu ya Afya Moja kwa kushirikiana na washirika (AFROHUN) ni pamoja na kuanzisha mitaala ya mafunzo kwa wafanyakazi wa afya na moduli za vyuo vikuu kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza.

### 2.5.2 Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Tanzania bara, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina jukumu la kusimamia afya ya wanyama na kulinda Afya ya jamii dhidi ya hatari za kiafya zitokanazo na wanyama. Wizara imeweka mifumo ya Kitaifa, Kikanda, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kata na Vijiji ili kurahisisha usimamizi wa masuala ya afya ya wanyama kama vile ufuatiliaji, utambuzi, kinga na udhibiti wa magonjwa. Katika ngazi ya Taifa, Serikali imeanzisha Kurugenzi ya Huduma za Mifugo ndani ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kusimamia masuala ya afya ya wanyama. Aidha, upo mfumo wa maabara ya mifugo unaosimamiwa na Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania (TVLA) kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara wa magonjwa ya mifugo na vyakula vya mifugo. TVLA pia huzalisha chanjo za Mifugo na kufanya tafiti katika magonjwa ya wanyama. Aidha, kuna maabara nyingine za Serikali zinazomilikiwa na taasisi kama SUA, NM-AIST, LITA, TALIRI na TAWIRI.
Kuna Vituo vinane vya Kanda vya Mifugo vinavyosimamiwa na Kurugenzi ya Huduma za Mifugo na kuna vituo 11 vya kanda vya TVLA nchini . Ufuatiliaji wa Magonjwa unafanywa na ZVC na vituo vya TVLA kwa kushirikiana na Daktari wa Mifugo wa Mikoa na Wilaya. Shughuli za kuzuia na kudhibiti magonjwa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya husimamiwa na maofisa wa ZVC. Daktari wa Mifugo wa Mikoa, Wilaya na maofisa mifugo wa Kata/Vijiji wanawajibika kuchukua hatua zote muhimu za kuzuia na kudhibiti magonjwa ya wanyama na zuonotiki. Sehemu ya huduma za mifugo katika ngazi hizi hutolewa na sekta binafsi.

Mlipuko au tukio la ugonjwa wa mifugo shambani huripotiwa na mkulima au mtoa huduma wa afya ya mifugo kwa ofisa mifugo aliye karibu naye (ofisa mifugo wa kijiji au kata). Mtiririko wa taarifa hizo hupelekwa kwa Daktari wa mifugo wa Wilaya, Mkoa, Vituo vya Kanda vya Mifugo, vituo vya TVLA na hatimaye kwa Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo).
Iwapo ni kwa magonjwa yanayoweza kutambuliwa, Kurugenzi ya Huduma za Mifugo huripoti kwa Ofisi ya Waziri Mkuu (OWM) , Shirika la Afya ya Wanyama Duniani, EAC na SADC. Aidha, Kurugenzi ya Huduma za Mifugo inapata taarifa za magonjwa wa zuonotiki kutoka Wizara ya Afya na magonjwa ya wanyamapori kutoka Wizara ya

Maliasili na Utalii. Utoaji wa taarifa za matukio na milipuko ya magonjwa hufanyika kwa njia ya taarifa za wiki na mtandao-(EMA-i) unaotumia simu ya mkononi.

### 2.5.3 Wizara ya Maliasili na Utalii

Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa jukumu la kufanya ufuatiliaji wa magonjwa ya kuambukiza kwa wanyamapori *kwenye* maeneo yaliyohifadhiwa ya makundi *tofauti* na kwenye mifumo ya ikolojia nchini. Haya yanatekelezwa kupitia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) na msimamizi wa maeneo ya hifadhi ya wanyamapori ambaye ni Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) imepewa jukumu la kuratibu na kufanya utafiti kuhusiana na wanyamapori nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Sheria ya TAWIRI, pamoja na mambo mengine, kipengele cha 5 kinaitaka taasisi hiyo kufanya utafiti na uchunguzi wa magonjwa ya wanyamapori ili kujua sababu na kupendekeza njia za kuyadhibiti.

TAWIRI ndiyo taasisi inayoongoza kwa masuala yote ya kitaalamu yanayohusiana na utafiti, afya na ustawi wa wanyamapori nchini Tanzania. TANAPA, NCAA na TAWA ni mamlaka za usimamizi zinazohusika na uhifadhi wa wanyamapori - mimea, wanyama na mazingira katika maeneo ya hifadhi ya wanyamapori yaliyo chini ya mamlaka yao. Hawa ni wasimamizi na walinzi wa rasilimali zote katika maeneo wanayosimamia ikiwa ni pamoja na mimea, wanyama na makazi yao. Katika kutekeleza wajibu wao, taasisi hizi hufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi husika. Kwa hiyo, TAWIRI, TANAPA, NCAA, TAWA kwa kushirikiana na jamii zinazowazunguka katika maeneo mbalimbali ya hifadhi ya wanyamapori wana wajibu wa kuweka mikakati ya kujikinga na kudhibiti magonjwa ambukizi na yasiyo ya kuambukiza kwa wanyamapori.

Takriban asilimia 38 ya ardhi katika nchi hii imetengwa kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori katika mfumo wa Hifadhi za Taifa 22, Hifadhi ya Ngorongoro 1, Mapori ya Akiba 32, Mapori ya Hifadhi ya Wanyamapori 16, Mapori Tengefu 38 na maeneo ya wazi. Pia, kuna misitu ya asili 13, mashamba ya misitu 21 na sehemu ndefu ya misitu ya mikoko katika maeneo ya mashariki mwa nchi kando ya Pwani ya Bahari ya Hindi (URT, 2021). Maeneo haya yana mandhari na hali ya hewa tofauti ambayo inawezesha kuwapo kwa utofauti mkubwa wa, mimea na wanyama. Misitu, milima, pori la savana, mabonde ya ufa, milima mikubwana midogo katika maeneo tambarare, ardhi oevu, maziwa, mito, vijito na nyanda fupi za nyasi kwenye mandhari haya hutoa makazi ya kipekee yenye mahitaji mengi ya kimsingi ya maisha (chakula, na malazi) ya aina mbalimbali za wanyamapori, ikijumuisha wanyama wakubwa, mamalia wadogo, wadudu, viumbe vya majini, ndege na mimea mbalimbali. Pamoja na utofauti huo mkubwa, maeneo yaliyohifadhiwa pia ni makazi ya vijidudu mbalimbali vikiwemo virusi, bakteria, fangasi na protozoa ambao baadhi yao wanahusika na magonjwa mbalimbali ya wanyama na watu.

#### 2.5.3.1 Muundo wa Kiutawala

Katika kuchunguza magonjwa ya wanyamapori, madaktari wa mifugo wanaofanya kazi na Mamlaka mbalimbali za Usimamizi wa Wanyamapori ambazo ni TANAPA, NCAA, TAWA na TAWIRI hutoa taarifa kwa wakuu ndani ya taasisi husika kupitia taratibu za mawasiliano zilizowekwa. Daktari wa wanyamapori anaripoti kwa Ofisa msimamizi wa eneo lililohifadhiwa na kwa wakuu wa taasisi. Maofisa hao, wanafanya kazi kwa kushirikiana na Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania (TVLA) na Vituo vya Kanda vya Mifugo ambavyo viko chini ya DVS na Ofisa Mfawidhi wa ZVC huripoti

kwa DVS. Kwa hiyo, magonjwa yanayogunduliwa ya wanyamapori yakiwemo magonjwa ya endemiki, yanayoibuka na yanayojirudia na yale ya zuonotiki kutoka nchi nzima yanaripotiwa kwa DVS katika Wizara yenye dhamana ya Mifugo. Kwa mujibu wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama namba 17 ya 2003, utoaji wa taarifa za milipuko ya magonjwa kwa kawaida hufuatiliwa kwa karibu ili kuwezesha uandaaji wa taarifa kwa wakati kwa mamlaka za juu ili iweze kuandaa rasilimali na kuweka mipango ya kukabiliana nayo.

#### 2.5.3.2 Mifumo ya Ufuatiliaji, Utambuzi na Udhibiti wa Magonjwa ya Wanyamapori

Wanyamapori wanakufa kwa magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza sawa na viumbe hai wengine. Vimelea vya magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na virusi, bakteria, protozoa, fangasi, vinahusika na magonjwa mbalimbali ya kuambukiza kwa wanyamapori. Baadhi ya magonjwa yanajulikana kuwa miongoni mwa sababu za kuangamiza na kutoweka kwa spishi za wanyamapori, hasa zile zilizo hatarini kutoweka kwani zinahusishwa na magonjwa makali. Miongoni mwao ni Sotoka, Kimeta, *Canine Distemper*, Kichaa cha mbwa, na Mafua Makali ya Ndege. Baadhi ya spishi za wanyamapori zinajulikana kuwa hifadhi ya vimelea vya magonjwa ambavyo husababisha maambukizi kutoka kwa wanyamapori hadi kwa binadamu hasa wale wanaoishi kwenye maeneo ya mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori. Vilevile, magonjwa mengine yanaambukizwa kutoka kwa wanadamu kwenda kwa wanyamapori. Kulingana na hali ya asili ya vimelea na mazingira wezeshi, ugonjwa unaweza kuenea mbali zaidi. Kwa mfano, ugonjwa unaosababishwa na virusi kama vile homa ya dinga, homa ya manjano, Zika, chikungunya na virusi vya Nile Magharibi (Weaver, 2013). Magonjwa mengine ni pamoja na: Kimeta, Brusilosisi , kifua kikuu, Mafua ya ndege, Kichaa cha mbwa, Homa ya bonde la ufa, malale na minyoo k.m Ekimokokasi (*Echnococcosis)*, Tegu *(Taeniosis)* na Askari *(ascariosis)*.

#### 2.5.3.3 Mfumo wa Maabara

Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii zina aina mbili za maabara za mifugo. Kwanza, maabara ya msingi ya mifugo ambayo iko katika eneo husika lililohifadhiwa au katika maabara ya kanda ya mifugo, ambayo huhudumia maeneo kadhaa yaliyohifadhiwa. Kimsingi ni maabara za Kiwango cha Usalama wa Mazingira (BSL) 1 zilizo na vifaa vya msingi na zana za kufanyia kazi ili kushughulikia ukusanyaji wa sampuli, uchakataji wa awali, uchunguzi, uhifadhi wa muda, ufungashaji na usafirishaji kwenda maabara ya juu zaidi. Maabara zote za mifugo zilizoko kimkakati katika uwanja wa TAWIRI, TANAPA na NCAA ziko chini ya aina hii (BSL 1). Pili, maabara ya mifugo ya BSL 2 ipo Makao Makuu ya TAWIRI jijini Arusha, ikiwa ni rufaa kwa maabara za msingi zilizo chini yake (BSL 1). Maabara nyingine ya mifugo ya BSL 2 iko mbioni kujengwa na TANAPA jijini Arusha. Maabara hii itatumika kama rufaa kwa maabara zote za msingi katika mfumo wa TANAPA. Maabara za mifugo za BSL 2 hupokea sampuli kutoka kwa maabara za BSL1, kwa ajili ya kuzichakata zaidi, kufanya uchunguzi, kuhifadhi sampuli kwa muda mrefu, kuweka kumbukumbu, kufungasha na kusafirisha sampuli za wanyamapori kwenda maabara *za* juu za mifugo ndani na nje ya nchi. Maabara zote hizi zinafanya kazi kwa ushirikiano na TVLA na ZVC ambazo ziko kimkakati nchini.

### 2.5.4 Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

Moja ya majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni usimamizi wa mazingira asilia kwa manufaa ya afya ya binadamu na mfumo wa ikolojia kwa ujumla. Usimamizi wa mazingira unahakikisha uendelevu na matumizi sawa ya rasilimali katika kushughulikia mahitaji ya msingi ya kizazi cha sasa na kijacho bila kuharibu mazingira. Mazingira borani mazuri kwa afya kwani yanapunguza uwezekano wa ulemavu, magonjwa na vifo, kuboresha hali ya lishe na kuongeza muda wa kuishi. Imetafitiwa kuwa ni mazingira salama ni muhimu katika kudhibiti baadhi ya magonjwa. Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri ubora wa maji jambo ambalo ni tatizo kubwa katika sekta ya afya kwani watu wanaugua magonjwa yatokanayo na maji kama vile malaria, kuhara, kipindupindu na homa ya dinga. Haya yanahusishwa zaidi na kuongezeka kwa mvua na halijoto kutokana na mabadiliko ya tabianchi duniani.

### 2.5.5 Wizara ya Kilimo

Tanzania bara, Huduma za Afya ya Mimea (PHS) chini ya Wizara ya Kilimo zinafanya kazi katika ngazi mbalimbali zinazojumuisha ngazi ya Taifa, Kanda, Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji. Katika ngazi ya Taifa, Mkurugenzi Msaidizi wa Afya ya Mimea (AD-PHS) anawajibika kwa masuala yote yanayohusu afya ya mimea kama vile wadudu na magonjwa, ufuatiliaji, kutambua wadudu na magonjwa, kuzuia na kudhibiti. PHS ipo kwa ajili ya kulinda afya ya binadamu kwa kudhibiti wadudu, magonjwa na mazingira; kuweka mikakati na mbinu shirikishi za Kudhibiti Wadudu (IPM) ili kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna.

Kuna kanda tano za PHS (Mashariki, Kati, Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini na Ziwa/Magharibi) na vituo vitatu maalumu (Udhibiti wa panya, udhibiti wa viumbe hai na Kilimo Anga). Inapotokea magonjwa au mlipuko wa wadudu kama vile Aflatoksini, Nzige na Kwelea , viwavijeshi (Fall Armyworm) huripotiwa na Wafanyakazi wa Ugani wa Kijiji ama kwa Maofisa wa Ulinzi wa Mimea wa Wilaya (DPPOs) wa Vituo vya Afya vya Wilaya/Kanda husika au kwa AD-PHS kwa hatua zaidi. Shughuli za kuzuia na kudhibiti wadudu katika ngazi ya Mkoa na Wilaya zinasimamiwa na mratibu wa Afya ya Mimea wa Kanda.

Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Kata/vijiji wanachukua hatua zinazohitajika katika kuzuia na kudhibiti Wadudu waharibifu ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji, kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu utambuzi na udhibiti wa wadudu waharibifu kutumia Mbinu Jumuishi ya Kudhibiti Wadudu (IPM).Taarifa ya uvamizi wa wadudu shambani hutolewa na mkulima kwa Ofisa Ugani wa Kijiji aliye karibu. Mtiririko wa taarifa hizo huelekezwa kwa DPPO, Mratibu wa Kanda, na hatimaye kwa AD-PHS katika ngazi ya Wizara. Ikiwa wadudu hao wapo kwenye orodha maalumu ya wale wanaotakiwa kutolewa taarifa, taarifa hutolewa kwa kuzingatia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Wadudu (IPPC) na Ofisa wa Kitaifa wa Ulinzi wa Mimea (NPPO). Taarifa rasmi ya uvamizi wa wadudu hutolewa kwa njia ya baruapepe/simu.

Wadudu, wanyama na magonjwa muhimu yanayotishia uchumi na kuathiri binadamu, wanyama na mimea nchini Tanzania ni pamoja na ndege wanaokula nafaka (kwelea kwelea) , nzige wekundu wa jangwani, viwavi jeshi, magonjwa ya kuvu na panya wa shambani. Wadudu na magonjwa haya hutangazwa kuwa uvamizi wa wadudu au ugonjwa wa mlipuko unapoathiri wakulima wengi na kusambaa katika maeneo makubwa ya ardhi

### 2.5.6 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) imepewa jukumu la kuandaa Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu, Ujuzi, Maendeleo ya Mafunzo na utekelezaji wake. Hivyo inatazamiwa kuwa Wizara inasimamia taasisi za elimu na mafunzo kwa ujumla pamoja na kusimamia shughuli za utafiti zinazohusu masuala mtambuko ya afya ambayo yanahusu Mtazamo wa Afya Moja. Wizara pia inasimamia huduma za chakula, lishe na afya katika taasisi za elimu. Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inahakikisha kwamba watoto wenye mahitaji maalumu wanatambuliwa na kupatiwa huduma za urekebishaji kulingana na mahitaji yao. Ili kuhakikisha kuwepo kwa wanafunzi wenye afya bora, Wiizara itatoa elimu ifaayo ya afya ya uzazi na ujinsia kwa wanafunzi wote wakiwemo wale wenye mahitaji maalumu.

## 2.6 Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto (SWOC)

Uchambuzi wa kuangalia Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto (SWOC) ulifanyika ili kuainisha sababu za sasa za ndani na nje (sheria, ufadhili, magonjwa yanayoibuka na teknolojia mpya) katika mazingira ya utendaji zinazoweza kuathiri utekelezaji wa mbinu ya Afya Moja. Matokeo ya uchambuzi yameainishwa hapa chini.

### Jedwali Na 1: Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto (SWOC)

| Nguzo na 1: Uratibu | | | |
|---|---|---|---|
| **UWEZO** | **UDHAIFU** | **FURSA** | **CHANGAMOTO** |
| i. Kuanzishwa kwa Sehemu ya Afya Moja<br>ii. Kuwepo kwa wafanyakazi/watumishi wenye mafuno katika maeneo maalumu<br>iii. Kuwepo kwa wataalamu wa Afya Moja (wa fani nasekta mbalimbali)<br>iv. Utashi wa kisiasa kupitia OWM<br>v. Kuwepo kwa mipango ya dharura ya sekta mbalimbali (Mpango wa Taifa wa Mafua ya Ndege, mpango wa dharura wa RVF, Mpango wa kujiandaa na kukabili Hatari na Dharura kwa Afya ya jamii)<br>vi. Kuwepo kwa Juhudi za utekelezaji wa mbinu ya Afya Moja kwenye sekta mbalimbali kama - AFROHUN, SACIDS, Afrique One.)<br>vii. Kuwepo kwa kamati za Kikosi Kazi cha Kitaifa katika sekta mbalimbali zikiwemo za kukabiliana na matukio ya afya ya jamii ikiwa ni pamoja na | i. Ushirikiano usiotosha kati ya OHS na sekta zinazohusika<br>ii. Uelewa mdogo kuhusu magonjwa ya zuonosia, AMR na matishio mengine ya afya ya jamii miongoni mwa watunga sera, wanasiasa na jamii.<br>iii. Rasilimali chache za kusaidia Sehemu ya Afya Moja<br>iv. Utekelezaji hafifu wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Afya Moja<br>v. Ukosefu wa Sera ya Afya Moja<br>vi. Uhaba wa mafunzo ya kutosha kazini. | i. Ushirikiano baina ya WHO,OIE,FAO na UNEP katika utekeelzaji wa Afya Moja<br>ii. Kuwepo kwa mkataba wa silaha za kibiolojia ulioridhiwa (BWC, Itifaki ya Cartagena)<br>iii. Kuwepo kwa washirika wa maendeleo na usaidizi wa ndani (FAO, WHO, CDC)<br>iv. Kuwepo kwa washirika mbalimbali wa utekelezaji wa Afya Moja wa ndani | i. Mdororo wa kiuchumi duniani<br>ii. Kukosekana kwa utulivu wa kisiasa miongoni mwa nchi jirani<br>iii. Kuwepo kwa magonjwa yanayoibuka na kujirudia ya zuonotiki kama vile Ebola, UVIKO - 19 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| magonjwa ya zuonotiki (AMR, IHR)<br>viii. Ushirikiano imara miongoni mwa Wizara na taasisi kupitia TWG zilizoanzishwa<br>ix. Kuwepo kwa vyama vya kitaaluma kama vile TVA, TMA, TABSA. | | | |
| **Nguzo na 2 –Ufuatiliaji na utambuzi, Kinga na Udhibiti** | | | |
| **UWEZO** | **UDHAIFU** | **FURSA** | **CHANGAMOTO** |
| i. Kuwepo kwa sheria na sera<br>ii. Kuwepo kwa mifumo ya ufuatiliaji<br>iii. Kuwepo kwa miongozo ya ufuatiliaji kama (IDSR/IHR (2005), EBS; miongozo ya ufuatiliaji wa magonjwa ya zuonotiki yaliyopewa kipaumbele;. Mfumo wa Ufuatiliaji wa AMR (2018)<br><br>v. Mikakati ya kudhibiti magonjwa yaliyopewa kipaumbele<br>vi. Kuwepo kwa mipango ya dharura kwa baadhi ya magonjwa kama vile Mpango wa Dharura wa RVF, HPAI - H5N1, Ebola na UVIKO - 19<br>vii. Kuwepo kwa miundombinu ya maabara yenye wataalamu wenye | i. Kukosekana kwa sera shirikishi ya maabara baina ya sekta<br>ii. Ukosefu wa sera ya Kitaifa ya Afya Moja<br>iii. Uratibu ushirikiano na mawasiliano yasiyotosheleza miongoni mwa sekta<br>iv. Upungufu wa uwezo wa maabara katika ngazi ya chini kwa sekta mbalimbali (afya, mifugo, wanyamapori)<br>v. Uwezo usiotosheza wa rasilimali watu katika ngazi za chini<br>vi. Ushirikishwaji na ushiriki mdogo wa jamii katika ufuatiliaji na kutoa taarifa<br>vii. Ushirikishanaji usiotoshelea wa data za ufuatiliaji magonjwa miongoni mwa sekta | i. Kuwepo kwa washirika wanaosaidia kufuatilia kuzuia na kudhibiti magonjwa<br>ii. Kuwepo kwa jitihada ya utekelezaji wa Afya Moja, kikanda, na kimataifa (AFROHUN, SACIDS, SADC, AU, SNL, BTRP, DTRA, GIZ)<br>iii. Kuwepo kwa Mpango Mkakati wa EAC wa Afya Moja; Kuwepo kwa miongozo elekezi inayotambulika kimataifa (OIE, FAO, WHO)<br>iv. Kuwepo kwa maabara za marejeo za kimataifa kwa magonjwa maalum) | i. Magonjwa ya zuonotiki yanayoibuka na kujirudia.<br>ii. Hali ya hewa isiyotabirika / mabadiliko ya tabianchi<br>iii. Kuwepo kwa mipaka isiyodhibitika (njia za panya)<br>iv. Utegemei kwa wafadhili<br>v. Mgongano wa maslahi katika kuweka vipaumbele miongoni mwa washirika wakuu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| sifa<br>viii. Watumishi wenye mafunzo na uwezo katika ngazi ya Taifa na ngazi za chini<br>ix. Miundombinu bora ya mawasiliano<br>x.Kuwepo kwa TEHAMA ambayo inasaidia kuripoti kwa kutumia simu ya mkononi<br>Xi. Kuwepo kwa zana mbalimbali za ufuatiliaji<br>xii. Kuwepo kwa Kamati za Kitaifa na vikosi kazi vya IHR, AMR<br>xiii. Kuwepo kwa sekta binafsi inayosaidia ufuatiliaji | viii. Mrejesho usiotosheleza wa data za ufuatiliaji kati ya sekta na wakulima/wafugaji<br>ix. Uwezo usiotosheleza wa usimamizi, uchunguzi, uchambuzi na tafsiri wa data za ufuatiliaji<br>x. Utekelezaji hafifu wa mikakati iliyojumuishwa, taratibu a viwango vya utendaji (SoP) na miongozo inayosimamia magonjwa ya zuonotiki na zana zingine<br>Xi. Ushirikishwaji wa jamii usiotosheleza<br>xii. Uwezo mdogo wa kuandaa zana za uchunguzi na vitendanishi vya maabara.<br>xiii. Upatikanaji usiotosheleza waTEHAMA katika maeneo mengi nchini | | |
| **Nguzo na 3: Utayari na Uwezo wa Kukabili matukio** | | | |
| **UWEZO** | **UDHAIFU** | **FURSA** | **CHANGAMOTO** |
| i. Hali ya utulivu wa kisiasa na uungwaji mkono<br>ii. Kuwepo kwa miundo na mifumo ya maabara iliyofafanuliwa.<br>iii. Kuwepo kwa Mifumo ya Kudhibiti Matukio (IMS) na Vituo vya Uendeshaji wa Dharura katika | i. Uwezo mdogo wa usambazaji wa mipango ya Taifa ya Kujiandaa na kukabiliana na dharura kwa sekta zote kuanzia ngazi ya chini hadi Taifa.<br>ii.Ushirikishwaji usiotosheleza wa kamati za kukabiliana katika sekta | i. Kuwepo kwa washirika mbalimbali wa ndani wa utekelezaji wa Afya Moja<br>ii. Nia ya wafadhili/washirika kusaidia shughuli za kujiandaa na kukabili | i. Mgongano wa maslahi kwenye upangaji wa vipaumbele miongoni mwa wahusika wakuu<br>ii. Mdororo wa kiuchumi duniani kutokana na mlipuko unaoendelea wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| iv. Kuwepo kwa kamati za Maafa na Dharura<br>v. Kuwepo kwa Uratibu rasmi wa Sekta mbalimbali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Sehemu ya Afya Moja)<br>vi. Kuwepo kwa wataalamu wa fani na sekta mbalimbali<br>vii. Kuwepo kwa mipango mahususi ya hatari na magonjwa kwa sekta mbalimbali (Mipango ya Kitaifa ya Mafua ya Ndege, mpango wa dharura wa RVF, Mpango wa kukabiliana na Hatari na Dharura za Afya ya jamii)<br>viii. Kuwepo kwa kamati za Kikosi Kazi cha Kitaifa katika sekta mbalimbali za kukabiliana na matukio ya afya ya jamii yakiwemo magonjwa ya zuonotiki<br>ix. Kujumuisha masualambinu ya Afya Moja ndani ya sekta za serikali na katika mtaala wa mafunzo wa Chuo Kikuu<br>x. Wajibu wa nchi kuhusu Maazimio ya Kikanda na Kimataifa (IHR, GHSA) | iii. Vituo vichache vya Uendeshaji wa Dharura za kisekta katika ngazi chini<br>iv. Uwezo mdogo wa rasilimali watu kusaidia sekta mbalimbali katika kujiandaa na kukabili magonjwa yanayoibuka na kujirudia.<br>v. Mgongano wa wa vipaumbele miongoni mwa sekta hasa wakati wa kujiandaa na kukabili dharura<br>vi. Upungufu wa utaalamu katika kukabiliana na magonjwa yanayoibuka | iii. Kuwepo kwa jitihada za utekelezaji wa mbinu ya Afya Moja ya Kikanda na Kimataifa | iii. Kukosekana kwa utulivu wa kisiasa miongoni mwa nchi jirani |

| Nguzo na 4: Utafiti na Maendeleo | | | |
|---|---|---|---|
| **UWEZO** | **UDHAIFU** | **FURSA** | **CHANGAMOTO** |
| i. Kuwepo kwa majukwaa na mitandao ya uendeshaji wa Afya Moja ii. Mpango Mkakati wa Afya Mmoja uliozinduliwa mwaka 2018;<br>iii. Kuwepo kwa Sehemu ya Afya Moja<br>iv. Kuwepo kwa mifumo ya ufuatiliaji wa hatari na kukabiliana na dharura.<br>v. Kuwepo kwa wataalamu wa tafiti mbalimbali za kisekta<br>vi. Kuwepo kwa utashi wa kisiasa kuhusu thamani ya utafiti wa Afya Moja<br>vii. Kuwepo kwa rasilimali mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya utafiti k.m. wanyamapori, kilimo na mazingira.<br>viii. Kuwepo kwa taasisi za mafunzo zinazohusiana na Afya Moja<br>ix. Kuwepo kwa ushirikiano imara kati ya taasisi za utafiti na za maendeleo<br>x. Kuwepo kwa Mpango wa Afya Moja uliooanishwa na mtaala wa CPD miongoni mwa taasisi | i. Kiasi kidogo na ubora wa kiwango cha chini wa tafiti za Afya Moja (OH)<br>ii. Ufadhili mdogo wa kusaidia tafiti za OH<br>iii. Idadi ndogo ya rasilimali watu na miundombinu ya kusaidia tafiti za Afya Moja<br>iv. Ushirikiano mdogo miongoni mwa watafiti wa taasisi tofauti za kitaifa na kimataifa | i. Kuwepo kwa mashirika ya ufadhili ya nje<br>ii. Hali ya kuvutiwa kwa washirika wa maendeleoiii. Kuwepo kwa jukwaa la Afya Moja la Jumuiya ya Afya Mashariki iv. Kuwepo kwa majukwaa ya usambazaji wa utafiti<br>v. Kuwepo na matumizi ya teknolojia mpya<br>vi. Usajili na uidhinishaji wa mikataba na itifaki za kimataifa na kikanda (JEE, GHSA IHR). | i. i. Mdororo wa kiuchumi duniani<br>i. Matishio ya mara kwa mara ya magonjwa yanayoibuka na na kujirudia.<br><br>iii. Utegemezi mkubwa wa ufadhili wa nje kwa utafiti. |

| Nguzo na 5: Mafunzo , Utetezi  na Mawasiliano | | | |
|---|---|---|---|
| **UWEZO** | **UDHAIFU** | **FURSA** | **CHANGAMOTO** |
| i. Kuwepo kwa utaalamu wa sekta mbalimbali katika afya ya binadamu, wanyama na mazingira<br>ii. Upatikanaji wa nyaraka za Afya Moja<br>iii. Kuwepo kwa kikosi kazi cha uhamasishaji, utetezi na mawasiliano katika Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja<br>iv. Kuwepo kwa mkakati wa kitaifa wa mawasiliano wa AMR | i. Utaratibu dhaifu wa  kushirikishana taarifa za Afya Moja miongoni mwa Wizara za sekta, na wadau wengine husika<br>ii. Ukosefu wa Uelewa wa Afya Moja, mwongozo na mkakati wa utetezi na mawasiliano. , iii. Upungufu wa rasilimali watu na fedha kwa shughuli za uhamasishaji, utetezi na mawasiliano.<br>iv. Utetezi mdogo wa Afya Moja kwa watunga sera<br>v. Kutothaminiwa kwa dhana ya Afya Moja kwa watunga sera.<br>vi. Mgongano wa Maslahi katika kupanga vipaumbele miongoni mwa wahusika wakuu na mashirika kuhusu ufahamu, utetezi na mawasiliano.<br>vii. Kutegemea washirika wa maendeleo katika programu za uhamasishaji, , utetezi na mawasiliano za Afya Moja.<br>viii. Nyenzo chache za kuhamasisha Afya Moja<br>ix. Ukosefu wa mifumo ya ushirikishanaji wa data na habari kuhusu Afya Moja .<br>x. Uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala mbalimbali ya Afya Moja. | i. Kuwepo kwa mkakati wa kitaifa wa mawasiliano wa AMR<br>ii. Kuwepo kwa njia tofauti za kidigiti za mawasiliano (njia za mitandao ya kijamii)<br>iii. Kuwepo kwa AZAKI na washirika wa maendeleo wanaovutiwa na Afya Moja kwa mfano Programu ya RBA<br>iv. Kuwepo kwa programu za sekta ya Afya Moja<br>v. Kuwepo kwa majukwaa ya mawasiliano | i. Ubadilishaji wa vipaumbele na rasilimali zilizopangwa kwa shughuli za Uhamasishaji , Utetezi na mawasiliano ya Afya Moja kutokana na mienendo ya kitaifa na kimataifa. |

| ***Nguzo Na.* 6: *Mafunzo na Elimu*** | | | |
|---|---|---|---|
| **UWEZO** | **UDHAIFU** | **FURSA** | **CHANGAMOTO** |
| i. Kuwepo kwa taasisi za mafunzo zinazoshughulikia afya ya binadamu, wanyama na mazingira<br>ii. Kuwepo kwa utaalamu wa sekta mbalimbali katika afya ya binadamu, wanyama na mazingira<br>iii. Kuwepo kwa kozi za mafunzo tarajali zilizojumuishwa za Afya Moja<br>iv. Kuwepo kwa programu jumuishi za mafunzo ya kujiendeleza ya Afya Moja katika vyuo vya kitaaluma na taasisi za elimu ya juu.<br>v. Kuwepo kwa nyenzo za kufundishia (mitaala, vitabu vya kiada na miongozo)<br>vi. Upatikanaji wa nyaraka kuhusu Afya Moja. | i. Ukosefu wa mpango wa mafunzo ya Afya Moja<br>ii. Nyenzo chache za kusaidia mafunzo ya kielektroniki ya Afya Moja (vitabu vya sauti, miundo ya kuigiza)<br>iii. Upungufu wa rasilimali watu na fedha<br>iv. Kutegemea washirika wa maendeleo katika programu za mafunzo ya Afya Moja,<br>v. Kuchelewa kutumia Mbinu ya Afya Moja miongoni mwa watunga sera, maofisa watendaji na wasimamizi.vi. Uelewa mdogo wa Mbinu ya Afya Moja kwa watunga sera, Maofisa Watendaji na Wasimamizi | i. Kuwepo kwa mabaraza ya kitaaluma yenye uwezo nchini Tanzania (*MCT, VCT)*<br>ii. Kuwepo kwa Mashirika ya Udhibiti (*TCU, NACTE, CGLA, TMDA*)<br>iii. Kuwepo kwa programu za CPD nchini Tanzania<br>iv. Kuwepo kwa majukwaa ya mafunzo ya kielektroniki ( ECHO, ZOOM)<br>v. Kuwepo kwa programu za Afya Moja kwenye Wizara za kisekta<br>vi. Mahitaji makubwa ya kujenga uwezo katika utekelezaji wa mbinu ya Afya Moja | Utegemezi mkubwa wa ufadhili wa nje kwa afua za Afya Moja |

## 2.7 Uchambuzi wa Wadau

### 2.7.1 Malengo ya kuwatambua Wadau wa Afya Moja

Malengo ya kuwatambua wadau wa Afya Moja ni kuibua wadau kwa, kuonesha uhusiano, ushirikiano, mawasiliano na ushawishi wao katika shughuli za Afya Moja nchini kwa kushirikiana na Sehemu ya Afya Moja (OHS) . Matokeo ya uchambuzi yatatumika kuongoza ushiriki wa wadau wakati wa utekelezaji wa shughuli za Afya Moja

### 2.7.2 Kielelezo Dhahiri cha Wadau

Uchambuzi wa mdau mmojammoja wa Afya Moja ulifanywa ili kutathmini mwingiliano na ushawishi. Matokeo yalionesha kuwa wadau wengi walikuwa na mwingiliano mkubwa na Sehemu ya Afya Moja (OHS). Aidha, walikuwa na ushawishi wa hali na mali kwenye shughuli za utekeleaji wa mbinu ya Afya Moja. Hata hivyo, kundi lenye ushawishi mkubwa zaidi kwa raslimali lilikuwa ni AZISE na taasisi za kimataifa. Viongozi wa kisiasa na vikundi vya kidini vilikuwa na ushawishi mkubwa, wakati jamii ilikuwa na mwingiliano mdogo na OHS. Vilevile, jumuiya na vyama vya kitaaluma vilikuwa kwenye kundi lenye mwingiliano na ushawishi mdogo kuliko yote., Aidha, vyombo vya habari vilikuwa na mwingiliano wa chini na OHS lakini ushawishi wao ni mkubwa. Mkakati wa mawasiliano na utetezi unatakiwa kuandaliwa kwa kuzingatia matokeo ya kielelezo dhahiri cha wadau. Kielelezo ni kama kinavyoonekana hapo chini.




Kielelezo na. 1. *Kinaonesha mwingiliano na ushawishi kwa serikali kuu, TAMISEMI, jumuiya na vyama vya kitaaluma, sekta binafsi na vyombo vya habari. Ukaribu na OHS unaonesha mwingiliano imara, ukubwa wa duara unawakilisha kiwango cha ushawishi wa rasilimali. Vivuli vya rangi vinawakilisha kiwango cha ushawishi wa hali na mali; mkoleo mkubwa wa rangi unaonesha ushawishi mkubwa*

## 3. MPANGO MKAKATI

### 3.1 Kusudi

Kusudi la jumla la Mpango Mkakati ni kutoa mwelekeo wa kimkakati katika utekelezaji wa Ajenda ya Afya Moja (OH). Mpango unakusudia kuboresha utendaji wa OHS; kuboresha uwajibikaji; kuwa kama chombo cha mawasiliano ndani ya serikali na wadau wengine; kupanga muda wa utekelezaji; kuonesha jinsi ya kupima maendeleo ya utekeleaji wa mkakati; na kupanga maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya ugawaji wa rasilimali chache kwa ufanisi..

### 3.2.Dira na Dhamira

#### 3.2.1 Dira

Taifa lenye afya bora kwa watu, wanyama na mazingira, itakayopatikana kupitia juhudi za ushirikiano ndani ya nchi, kitaifa, kikanda na kimataifa.

#### 3.2.2 Dhamira

Kuboresha ustawi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhamasisha ushirikiano katika kushughulikia vipaumbele vya Afya Moja nchini.

### 3.3 Malengo ya Mkakati

Kutoa mifumo ya kiutendaji na ubora iliyounganishwa ya afya ya binadamu, wanyama na mazingira ili kupunguza changamoto zamatishio ya kiafya katika viwango vyote

### 3.4 Maadili ya Msingi

Yafuatayo ni maadili ya msingi yatakayoongoza utekelezaji wa Mpango Mkakati huu:

i. Ushirikiano - Kuhamasisha ushirikiano na kufanya kazi pamoja ili kuwa na nguvu ya umoja kwa manufaa ya wote;
ii. Kubadilika - ubunifu na usikivu ili kukidhi mahitaji yanayobadilika ya jamii yetu;
iii. Ubora - kuhamasisha utendaji kazi wa viwango vya juu zaidi katika mawanda ya Afya Moja ili kuhakikisha kuna maboresho endelevu ya viwango vyote;

iv. Utendaji Kazi wa pamoja - uhusiano wa karibu wa kufanya kazi na wadau wote kwa pamoja;
v. Uwazi - Ukweli na utayari wa kuhamasisha na kushiriki katika kutekeleza mbinu ya Afya Moja; na
vi. Ustahimilivu - kuwatambua wafanyakazi , programu, taaluma, sekta, na asili zao kwa madhumuni ya kufikia lengo lililokusudiwa.

### 3.5 Kanuni Elekezi

Kanuni zifuatazo zitaongoza utekelezaji wa mpango huu:
i. Uzuiaji na udhibiti wa zuonosia ni mkakati wa kitaifa unaoihitaji uwajibikaji wa kisiasa na kiuchumi katika ngazi ya kitaifa na ngazi za chini

ii. Utumiaji endelevu wa taasisi zilizopo na kila inapowezekana kutumia uzoefu uliopatika kutokana na matukio yaliyopita.

iii. Utumiaji wa mbinu za fani mbalimbali ili kutambua mifumo ya kisheria, kitaalamu, kisiasa, inayohitajika kudhibiti ipasavyo zuonosia.
iv. Kutumia uthibitisho wa kisayansi na kuendelea kupokea habari na teknolojia mpya
v. Kutambua na kuheshimu tofauti za kitamaduni.

### 3.6 Nguzo na Malengo ya Kimkakati

Nguzo za kimkakati ni maeneo mapana ya kuzingatia ambayo tunapaswa kuwekeza na kuyafanyia kazi ili kufanikisha dhamira yetu. Mpango Mkakati utatekelezwa kuleta matokeo katika nguzo sita. Kila Nguzo ina shabaha i, Malengo, Mikakati, na Viashirio Muhimu vya Utendaji kama ifuatavyo:

**Jedwali Na 2: Mfumo wa Mtiririko wa Kimantiki**

| **Nguzo ya kimkakati Na.1: Uratibu** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo la kimkakati: Kuimarisha Afya Moja na kuifanya Taasisi ya Kuratibu katika Ngazi zote** | | | | | |
| **Lengo mahsusi** | **Mkakati** | **Shabaha** | **Kazi** | **Kiashirio** | **Namna ya kupima kiashirio** |
| 1.1 Kuongeza uwezo wa utendaji kazi wa Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja | 1.1.1 Imarisha Vikundi Kazi vya Kitaalamu ili vifanye kazi na kuratibiwa vizuri | 1.1.1.1 Anzisha Vikundi Kazi vya Kitaalamu vya Afya Moja kufikia 2023 | i. Tambua na teua wajumbe wa Vikundi Kazi vya Kitaalamu | -Idadi ya Vikundi Kazi vya Kitaalamu vilivyoanzishwa<br>-Idadi ya wajumbe wa Vikundi Kazi vya Kitaalamu walioteuliwa | -Muhtasari wa kikao cha wadau wa Afya Moja<br>-Nakala ya barua za uteuzi<br>-Hadidu za rejea zilizoandaliwa |
| | | | ii. Endesha warsha ya kuandaa hadidu za rejea kwa Vikundi Kazi vya Kitaalamu | -Idadi ya mikutano iliyoitishwa | -Hadidu za rejea zilizoandaliwa |
| | | 1.1.1.2 Endesha mikutano ya robo mwaka kwa Vikundi Kazi vya Kitaalamu kufikia 2027 | i. Alika wadau waliotambuliwa | -Idadi ya mikutano iliyoitishwa | -Muhtasari wa mikutano ya Vikundi Kazi vya Kitaalamu |
| | | | ii. Andaa nyaraka za mkutano na rasilimali zinazohitajika | | |
| | | | iii. Endesha mikutano | | |
| | | 1.1.1.3 Endesha mikutano ya nusu mwaka ya timu za Kitaalamu za Afya Moja (OH) ya sekta mbalimbali kitaifa, kikanda na wilaya ifikapo 2027. | i. Alika wadau waliotambuliwa | Idadi ya mikutano iliyoitishwa ya nusu mwaka | Muhtasari wa mikutano ya nusu mwaka |
| | | | ii. Andaa nyaraka za mkutano na rasilimali zinazohitajika | | |
| | | | iii.Endesha mikutano | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 1.1.1.4 Andaa warsha za kujenga uwezo kwa Vikundi Kazi vya Kitaalamu ifikapo 2027 | i. Fanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo | Idadi ya wajumbe wa Vikundi Kazi vya Kitaalamu waliopata mafunzo | Ripoti za mafunzo |
| | | | ii. Tambua na wasiliana na taasisi za mafunzo | | |
| | | | iii. Endesha mafunzo | | |
| | 1.1.2 Andaa warsha za kuwajengea uwezo Watumishi wa Sehemu ya Afya Moja na waratibu viungo wa Afya Moja kutoka sekta mbalimbali.. | 1.1.2.1 Endesha warsha mbili za mafunzo ya kuwajengea uwezo kila mwaka. | i. Fanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo | Idadi ya Wafanyakazi wa Sehemu ya Afya Moja na waratibu viungo waliopata mafunzo. | Ripoti za mafunzo. |
| | | | ii. ii. Tambua wawakilishi na wasiliana na taasisi za mafunzo | | |
| | | | iii. Endesha mafunzo | | |
| 1.2 Kuongeza rasilimali ili kusaidia shughuli za Afya Moja | 1.2.1 Imarisha uhamasishaji na ugawaji wa rasilimali kutoka serikalini, washirika wa maendeleo na sekta binafsi. | 1.2.1.1 Andaa Mkakati wa Kukusanya Rasilimali ifikapo 2027 | i. Tambua wadau na kuandaa warsha | - Mkakati wa uhamasishaji wa rasilimali<br><br>-Kuwepo kwa rasilimali Watu na Fedha za kutosha katika ngazi zote | -Mkakati wa uhamasishaji wa rasilimali |
| | | | ii. Andaa rasimu ya waraka wa Mkakati wa Kukusanya Rasilimali | | |
| | | | iii. Sambaza waraka wa mkakati wa uhamasishaji wa rasilimali kwa wadau | | |
| | | | iv. Tekeleza Mkakati wa Kukusanya Rasilimali | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 1.2.1.2 Endesha mikutano ya kila mwaka ya kuhamasisha rasilimali baina ya wadau na washirika watekelezaji ifikapo 2027. | i. Alika wadau waliotambuliwa<br>ii. Tambua na gawa maeneo ya ufadhili<br>iii. Andaa nyaraka za mkutano na rasilimali zinazohitajika<br>iv. Panga matukio ya uhamasishaji wa rasilimali | Idadi ya matukio ya uhamasishaji wa rasilimali yaliyofanyika | Muhtasari wa Vikao Taarifa za fedha zilizokusanywa. |
| | | 1.2.1.3 Andaa programu na miradi ya kusaidia shughuli za Afya Moja ifikapo Juni, 2027 | i. Andaa Andiko la Mradi<br>ii. Panga na andaa mikutano ya Wadau | Idadi ya programu na miradi iliyoandaliwa | - Idadi ya programu na miradi iliyopata fedha |
| 1.3 Kuimarisha uhusiano kati ya Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja, na majukwaa ya kitaifa na kimataifa. | 1.3.1 Imarisha uhusiano wa kikazi kati ya Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja, majukwaa ya kitaifa na kimataifa. | 1.3.1.1 Andaa jukwaa la kitaifa la Afya Moja kwa kutumia muundo uliopo kufikia 2027 | i. Tambua na alika wadau<br>ii. Andaa nyaraka za mkutano na rasilimali zinazohitajika<br>iii. Endesha jukwaa la Taifa | -Idadi ya Mikutano iliyofanyika | |
| | | 1.3.1.2 Endesha mikutano ya robo mwaka ya watendaji wa OH katika ngazi za vijiji, kata, wilaya, mkoa na wizara ifikapo Juni, 2027. | i. Tambua na kualika wadau<br>ii. Andaa nyaraka za mikutano | -Idadi ya Mikutano iliyofanyika | - Ripoti za mikutano |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 1.3.1.3 Wezesha wafanyakazi wa Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja kuhudhuria mikutano ya Majukwaa ya Afya Moja ifikapo Juni, 2027 | Tambua idadi ya wafanyikazi wa Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja na tenga fedha kuwezesha mahudhurio yao ya mikutano ya Majukwaa ya Afya Moja. | -Idadi ya Mikutano waliyohudhuria<br>-Idadi ya wafanyakazi wa Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja walioshiriki.<br>Afya Moja | |
| **Nguzo ya Kimkakati Na 2: Ufuatiliaji, utambuzi, uzuiji na udhibiti wa magonjwa** | | | | | |
| **Lengo: Kuweka mifumo ya kiutendaji na bora ya ufuatiliaji wa pamoja wa afya ya binadamu na wanyama ili kupunguza athari za magonjwa ya zuonotiki , usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii.** | | | | | |
| **Lengo mahsusi** | **Mkakati** | **Shabaha** | **Kazi** | **Kiashirio** | **Namna ya kupima kiashirio** |
| 2.1 Kuimarisha ufuatiliaji wa pamoja, wa magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki , **usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii** katika ngazi zote. | 2.1.1 Anzisha mfumo wa pamoja wa ufuatiliaji wa magonjwa katika ngazi ya taifa, kanda/mkoa na wilaya kwa kutumia mbinu ya Afya Moja. | 2.1.1.1 Tengeneza miongozo, taratibu za viwango vya utendaji, miongozo ya ufuatiliaji wa magonjwa ya zuonotiki ya kipaumbele, **usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa** na matukio mengine ya afya ya jamii ifikapo 2027. | i. Tengeneza miongozo, taratibu za viwango vya utendaji , miongozo ya ufuatiliaji wa magonjwa ya zuonotiki ya kipaumbele, **usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa** na matukio mengine ya afya ya jamii | Idadi ya nyaraka za taratibu za viwango vya utendaji na miongozo kwa magonjwa ya zuonotiki ya kipaumbele, **usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa** na matukio mengine ya afya ya jamii | Kuwepo kwa taratibu za viwango vya utendaji na miongozo<br><br>Ripoti ya warsha<br><br>Ripoti ya usimamizi |
| | | | ii. Fanya warsha ya kusambaza miongozo ya Afya Moja | Idadi ya warsha zilizofanyika | |
| | | | iii. Fanya usimamizi shirikishi kwa wataalamu wa Afya Moja | Idadi ya kanda, mikoa na wilaya zinazosimamiwa | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | iv. Toa mafunzo kwa wataalamu wa afya ya binadamu na wanyama kuhusu ukusanyaji, uhifadhi na uchambuzi, wa data za ufuatiliaji wa pamoja wa magonjwa. . | | |
| | | | v. Tumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ukusanyaji wa data | | |
| | | | vi. Fanya uchunguzi shirikishi wa magonjwa ili kushirikisha jamii katika ufuatiliaji wa taarifa za matukio ya magonjwa | | |
| | | Toa mafunzo kwa watoa huduma wa afya ya binadamu na wanyama toka wilayani kuhusu ufuatiliaji wa magonjwa kwa kutumia mbinu ya Afya Moja kufikia 2027. | i. Endesha mafunzo ya magonjwa ya zuonotiki katika ngazi ya kanda, mikoa na wilaya. | Idadi ya wataalamu waliopatiwa mafunzo katika ngazi zote | Riti ya mafunzo |
| | | | ii. Endesha mikutano ya kila robo mwaka ya ufuatiliaji wa pamoja kuhusu magonjwa ya zuonotiki , usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii | Idadi ya Mikutano iliyofanyika | Ripoti ya Mikutano |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2.1.2 Imarisha ufuatiliaji wa pamoja wa magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na ufuatiliaji wa matishio ya afya ya jamii katika ngazi ya kitaifa, ukanda/mkoa, wilaya na jamii. | 2.1.2.1 Fanya tathmini ya pamoja ya hali hatarishi za magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawana matishio mengine ya Afya ya Jamii katika ngazi ya kanda, mikoa na wilaya ifikapo 2027 | i. Fanya tathmini ya pamoja ya hali hatarishi za magonjwa ya zuonotiki katika ngazi ya kanda, mikoa na wilaya<br>ii. Tekeleza mapendekezo husika. | Idadi ya watumishi waliofanya mafunzo ya tathmini ya pamoja ya hali hatarishi za magonjwa ya zuonotiki | Ripoti za mafunzo |
| | | 2.1.2.2 Fanya mikutano ya kila robo mwaka ya ufuatiliaji wa pamoja kuhusu magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii ifikapo 2027 | Endesha mikutano ya kila robo mwaka ya uchunguzi wa pamoja kuhusu magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii | Idadi ya mikutano iliyofanyika | Ripoti na muhtasari wa mikutano |
| | 2.1.3 Anzisha kanzidata ya pamoja katika Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja ya | 2.1.3.1 Wezesha Sehemu ya Uratibu wa Afya Moja, hifadhi na chambua data za ufuatiliaji wa pamoja kufikia 2027 | i. Fundisha wataalamu waSehemu ya Uratibu wa Afya Moja kuhusuukusanyaji, uhifadhi na uchambuzi ufuatiliaji wa pamoja | Idadi ya watumishi wa Sehemu ya Afya Moja waliopata mafunzo | Ripoti ya mafunzo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | magonjwa ya zuonotiki ,usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na matukio mengine ya afya ya jamii | | ii. Nunua na pakia programu ya uhifadhi na uchanganuzi wa data. | Upatikanaji wa programu | Kuwepo kwa Programu inayofanyakazi |
| | 2.1.4 Imarisha upashanaji wa taarifa za Nje ya mipaka ya nchi kwa magonjwa ya zuonotiki , usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine | 2.1.4.1Fanya mawasiliano ya hali hatarishi na ushiriki wa jamii kuhusu magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii ifikapo 2027. | i. Toa mafunzo ya Maarifa, Mtazamo na Vitendo kuhusu magonjwa ya zuonotiki , AMR na matukio mengine ya afya ya jamii | Idadi ya mafunzo ya Maarifa na Mtazamo (KAP) | Taarifa ya mafunzo ya Maarifa na Mtazamo (KAP) |
| | | | ii.Andaa na sambaza nyenzo na nyaraka za habari, elimu na mawasiliano kuhusu magonjwa ya zuonotiki , usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii<br><br>Toa mafunzo kwa jamii kuhusu magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii. | Idadi ya nyenzo za IEC zilizotolewa<br><br>Idadi ya waliopokea mafunzo | Nyenzo za IEC<br><br>Ripoti za mafunzo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | iii. Toa taarifa kuhusu kuzuia na kudhibiti magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii | Mafuzo yaliyotolewa | -Taarifa ya mafunzo<br>-Orodha ya washiriki |
| | | 2.1.4.2 Endesha vikao vya robo mwaka vya Kamati ya Ufuatiliaji wa Magonjwa yanayovuka mipaka ifikapo 2027 | Fanya tathmini ya pamoja ya *hali hatarishi* inayolenga magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii | Idadi ya mikutano iliyofanyika | Ripoti za mikutano |
| 2.2 Kuimarisha, kuzuia na kudhibiti magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki , usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na matishio mengine ya afya ya jamii katika ngazi zote. | 2.2.1 Imarisha uzuiaji na udhibiti wa magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki , usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii. | 2.2.1.1 Tekeleza mikakati ya udhibiti wawa magonjwa kipaumbele ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii.<br>, | i. Andaa na huisha miongozo na taratibu za viwango vya utendaji kwa chanjo za magonjwa ya zuonotiki ya kipaumbele | Idadi ya miongozo na SOP ziliyotengenezwa na kukaguliwa kwa kuzingatia magonjwa ya kipaumbele sita (6) PZD | Miongozo ipo |
| | | | ii. Nunua chanjo na vitendanishi vya kibiolojia. | Manunuzi ya dozi za chanjo na vitendanishi vya kibaiolojia | Ripoti za manunuzi |
| | | | iii. Fanya kampeni za uhamasishaji kabla ya chanjo. | Idadi ya kata na vijiji vilivyohamasishwa | Ripoti za uhamasishaji |
| | | | iv. Toa chanjo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele ya zuonotiki. | Idadi ya chanjo za magonjwa ya kipaumbele ya zuonotiki. | Ripoti za chanjo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | v. Fanya ufuatiliaji kabla na baada ya chanjo. | Idadi ya usimamizi shirikishi uliofanyika kabla na baada ya chanjo | Taarifa za ufuatiliaji |
| | | 2.1.2.2 Endesha mafunzo kazini kwa wafanyakazi kuhusu magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii ifikapo 2027. | i. Fanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo ya wafanyakazi | Idadi ya tathmini ya mahitaji iliyofanywa | Ripoti ya tathmini. |
| | | | ii. Endesha mafunzo kazini kwa wafanyakazi kuhusu kuzuia na kudhibiti magonjwa ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii. | Idadi ya wafanyakazi waliofundishwa | Ripoti za mafunzo |
| 2.3 Kuimarisha uwezo wa kutambua magonjwa ya *zuonotiki* ya kipaumbele katika ngazi ya kitaifa (100%), kanda/mikoa (60%) na wilaya (30%). | 3.1.1 Imarisha uwezo wa uchunguzi wa kimaabara | 3.1.1.1 Jenga uwezo wa maabara kwa sekta zote katika eneo la utambuzi wa magonjwa ya zuonotiki , usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na wa matukio mengine ya afya ifikapo 2027. | i. Fanya tathmini ya mahitaji ya maabara | Idadi ya tathmini zilizofanywa | Ripoti za tathmini |
| | | | ii. Nunua vifaa vya maabara, vitendanishi na vifaa tiba. | Idadi ya vifaa vya maabara, vitendanishi na vifaa tiba vilivyonunuliwa | Ripoti za vifaa |
| | | | iii. Toa mafunzo kwa wafanyikazi wa maabara katika sekta zote katika eneo la magonjwa ya zuonotiki , usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya kiafya | Idadi ya wafanyakazi waliofundishwa | Ripoti za mafunzo |
| | | | iv. Andaa taratibu za viwango vya utendaji ili kugundua magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya | Idadi ya taratibu za viwango vya utendaji zilizoandaliwa. | Taratibu za viwango vya utendaji zilizopo. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii | | |
| | | 3.1.1.2 Imarisha mtandao wa maabara wa sekta mbalimbali. | i. Andaa hadidu za rejea kwa ajili ya mitandao ya maabara.<br>ii. Endesha mikutano ya robo mwaka ya Kamati ya Sekta Mbalimbali yaUchunguzi wa Magonjwa, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii<br><br>iii. Fanya ulinganisho wa maabara kwa utambuzi wa magonjwa ya zuonotiki ya kipaumbele | Idadi ya hadidu za rejea zilizoandaliwa<br>Idadi ya mikutano iliyofanyika | Hadidu za rejea<br>Ripoti za Mafunzo ya wakufunzi<br><br>Ripoti za mikutano |
| | | 3.1.1.3 Imarisha menejimenti ya mfumo waubora wa huduma za maabara | i. Fanya ulinganisho wa matokeo miongoni mwa maabara kwa magonjwa ya zuonotiki ya kipaumbele | Idadi ya maabara zilizoshiriki kwenye ulinganisho wa matokeo<br><br>Kiwango cha ubora wa matokeo kwa asilimia | Ripoti ya ulinganisho |
| | | | ii. Fanya ukaguzi wa nje wa matokeo ya maabara kwa magonjwa zuonotiki ya kipaumbele. | Idadi ya ukaguzi wa nje uliyofanyika | Ripoti ya ukaguzi. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 3.1.1.4 Imarisha hatua za usalama na ulinzi wa kibiolojia dhidi ya vimelea hatarishi vya magonjwa katika maabara. | iii. Endesha mkutano wa usambazaji wa Miongozo ya usalama na ulinzi wa kibiolojia dhidi ya vimelea hatarishi vya magonjwa katika maabara. | Idadi ya mikutano iliyofanyika | Mihutasari ya Mikutano |
| | | | iv. Pitia upya orodhahakiki ya kitaifa ya usalama na ulinzi wa kibiolojia dhidi ya vimelea hatarishi vya magonjwa katika maabara. | Idadi ya orodhahakiki zilizopitiwa upya. | Orodha hakiki zilizopitiwa |
| | | | v. Tathmini utekelezaji wa usalama na ulinzi wa kibiolojia dhidi ya vimelea hatarishi vya magonjwa kwenye maabara sita kwa mwaka | Asilimia ya maabara zilizofanyiwa tathmini kwa mwaka. | Ripoti za tathmini. |
| | | | i. Endesha mafunzo ya usimamizi wa usalama na ulinzi wa kibiolojia dhidi ya vimelea hatarishi vya magonjwa kwenye maabara | Idadi ya mafunzo | Ripoti za mafunzo |
| **Nguzo ya kimkakati Na. 3: Kujiandaa na Kukabili Matukio** | | | | | |
| **Lengo la Kimkakati: Kuimarisha mifumo ya kujiandaa na kukabiliana mapema kwenye Sekta mbalimbali kwa kutumia mbinu ya Afya Moja** | | | | | |
| **Lengo mahsusi** | **Mkakati** | **Shabaha** | **Kazi** | **Kiashirio** | **Namna ya kupima kiashirio** |
| 3.1 Kuimarisha mifumo kwenye Sekta mbalimbali ya kujiandaa na | 3.1.1 Pitia upya mifumo iliyopo kwenye Sekta mbalimbali ya | 3.1.1.1 Pitia upya mifumo kwenye Sekta mbalimbali ya kujiandaa na | i. Tambua na ainisha wadau wakuu wa mchakato wa mapitio | -Idadi ya wadau waliotambuliwa na kuainishwa | Ripoti za mapitio |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| kukabiliana na matishio yanayohusiana na afya yanayoibuka na yanayojirudia. | kujiandaa na kukabiliana na matishio yanayohusiana na afya yanayoibuka na yanayojirudia. | kukabiliana kufikia 2027 | ii. Endesha warsha mbili kwa wadau wakuu ili kupitia upya mifumo iliyopo ifikapo 2027.. | Idadi ya warsha zilizofanyika<br><br>Idadi ya wadau waliohudhuria warsha | Ripoti za warsha<br><br>Usajili wa Mkutano |
| | | | iii. Endesha warsha moja ya wadau wakuu kuhakiki mifumo ifikapo 2027. | Idadi ya wadau walioshirki warsha ya uhakiki wa mifumo | Ripoti za warsha |
| | 3.1.2 Sambaza mifumo inayohusisha sekta mbalimbali ya kujiandaa na kukabiliana na matishio yanayohusiana na afya yanayoibuka na yanayojirudia | 3.1.2.1 sambaza mifumo iliyopitiwa upya na kuhakikiwa ya kujiandaa na kukabiliana na matishio yanayohusiana na afya yanayoibuka na yanayojirudia ifikapo 2027. | i. Andaa Warsha Moja ya mpango wa usambazaji | Mpango wa usambazaji umewekwa<br><br>Idadi ya watunga sera na washirika wa maendeleo waliohudhuria Warsha | Taarifa aya Warsha |
| | | | ii. Chapisha nakala 3000 za mifumo ya kukabiliana na dharura iliyohakikiwa | Idadi ya nakala | Taarifa za kupokea machapisho |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | katika ngazi zote. | | iii. Andaa Mikutano ya usambazaji kwa watunga sera na washirika wa Maendeleo kuhusu mifumo iliyopitiwa upya na kuhakikiwa. | Idadi ya washiriki na mikutano iliyoandaliwa | Ripoti za mikutano |
| | | | iv. Endesha Warsha kikanda na mikoani ili kusambaza na kugawa nakala za mifumo iliyopitiwa upya na kuhakikiwa. | Idadi ya warsha zilizoendeshwa | Usajili na ripoti za washiriki wa warsha |
| 3.2 Kuimarisha utendaji kazi wa mifumo ya kisekta ya kujiandaa na kukabiliana na changamoto zinazohusiana na afya zinazoibuka na zinazojirudia katika ngazi zote. | 3.2.1 Wezesha mazoezi ya pamoja ya kuigiza matukio mezani na uwandani kuhusu kujiandaa na kukabiliana na matishio yanayohusiana na afya yanayoibuka na yanayojirudia kwa kutumia mbinu ya Afya Moja kwenye ngazi za chini. | 3.2.1.1 Fanya mazoezi ya pamoja ya kuigiza matukio mezani na uwandani kwa wahusika wa sekta mbalimbali kwa ajili ya kujiandaa na kukabiliana na matishio yanayohusiana na Afya ifikapo 2027 | i. Fanya zoezi moja la pamoja la kuigiza matukio ya mezani kwa mwaka | -Idadi ya mazoezi ya pamoja ya kuigiza matukio kwa nyanja za juu (table top) yaliyofanyika kwa mwaka<br>-Idadi ya washiriki | Ripoti ya mazoezi yaliyofanyika<br><br>Idadi na usajili wa washiriki |
| | | | ii. Fanya zoezi moja la pamoja la kuigiza tukio la uwandani kwa mwaka | Idadi ya mazoezi ya pamoja ya kuigiza uwandani yaliyofanyika kwa mwaka<br>-Idadi ya washiriki | Ripoti ya mazoezi yaliyofanyika<br><br>Idadi na usajili wa washiriki |
| | | | iii. Endesha mkutano mmoja wa sekta mbalimbali kwa mwaka ili kuhuisha mpango kwa kutumia matokeo ya mazoezi ya kuigiza yaliyofanyika | -Idadi ya mikutano iliyofanyika | -Ripoti ya Mikutano<br><br>-Idadi na usajili wa washiriki |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | i. Fanya usimamizi shirikishi katika vituo vya kanda na mikoa kuhusu uendeshaji wa mifumo kujiandaa na kukabiliana na matukio kwenyesekta mbalimbali (Wasimamizi wawili kwa kila kituo) | -Idadi ya vituo vilivyotembelewa katika kilakanda na mkoa<br>- | -Ripoti ya kazi za zilizofanyika |
| | | | ii. Endesha mikutano miwili ya siku tatu kwa mwaka kwa washiriki 20 wa fani mbalimbali kuandaa bajeti | -Idadi ya mikutano iliyofanyika kwa mwaka<br>-Idadi ya washiriki wa fani mbalimbali walihudhuria | -Ripoti ya mikutano<br>-Orodha ya washiriki |
| | | 3.2.1.2 Imarisha Vituo vya Uendeshaji vya Dharura vya Mikoa vya sekta mbalimbali ili kusaidia mifumo ya kujiandaa na kukabiliana na matishio ya kiafya yanayoibuka na kujirudia ifikapo 2027. | i. Tambua na ainisha waratibu viungo wakuu wa sekta mbalimbali katika kila mkoa | -Idadi ya waratibu viungo wakuu waliotambuliwa na kuainishwa | -Ripoti ya utambuzi wa wahusika |
| | | | ii. Endesha warsha mbili za kuandaa mipango ya Kikanda ya Sekta mbalimbali Vituo vya Uendeshaji vya Dharura na taratibu za viwango vya utendaji | Idadi ya warsha zilizofanyika | Ripoti za warsha |
| | | | iii. Endesha warsha elekezi kwa waratibu viungo wa Vituo vya Uendeshaji vya Dharura kwenye sekta mbalimbali kuhusu taratibu za viwango vya utendaji | -Idadi ya warsha elekezi kwa waratibu viungo zilizoendeshwa<br>- Idadi ya washiriki<br>-Idadi ya sekta zilizohusika<br>- | -Ripoti ya Warsha<br>-Orodha ya washiriki |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | iv. Endesha mikutano ya usambazaji kimkoa kwa timu za usimamizi wa sekta mbalimbali kwenye wilaya | Idadi ya wilaya zilizoshiriki | -Ripoti za Mikutano ya Usambazaji |
| | 3.2.2 Hakikisha kuwepo kwa rasilimali watu ya kutosha (wa kukabiliana na matukio ya dharura) kwenye mifumo ya kukabiliana na changamoto za kiafya zinazoibukia na kujirudia katika sekta mbalimbali ngazi ya Kitaifa. | 3.2.2.1 Ajiri na elekeza rasilimali watu ya kutosha kwaajili ya mifumo ya kujiandaa na kukabiliana na matishio ya dharura ya kiafya yanayoibuka na kujirudia katika sekta mbalimbalikwenye ngazi za chini ifikapo 2027. | i. Fanya tathmini ya mahitaji ya rasilimali watu katika ngazi ya chini nchini | -Tathmini ya mahitaji iliyofanywa | -Ripoti ya tathmini |
| | | | ii. Andaa orodha ya pamoja ya wafanyakazi wanaohitajika kwa ajili ya kujiandaa na kukabiliana katika ngazi zote | -Orodha ya pamoja iliyoandaliwa | -Orodha ya watu waliopata mafunzo |
| | | | iii. Ajiri wafanyakazi wa kutosha kulingana na mahitaji katika ngazi zote ili kusaidia utayarishaji wa sekta mbalimbali na mifumo ya kukabiliana na matishio ya afya yanayojitokeza na kujirudia. | -Idadi ya wafanyakazi walioajiriwa.<br>-Sekta na fani za wafanyakazi walioajiriwa | -Orodha ya wafanyakazi walioajiriwa |
| | | | i. Endesha mafunzo elekezi kwa wafanyakazi kuhusu utayari wa sekta mbalimbali na mifumo ya kujiandaa na kukabiliana na matishio ya kiafya yanayoibuka na kujirudia, | - Idadi ya wafanyakazi waliopatiwa mafunzo | -Ripoti ya mafunzo<br><br>-Orodha ya washiriki |
| | | | | | |

| Ngazi ya Kimkakati Na. 4 Utafiti na Maendeleo | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Kimkakati – Kuimarisha Afya ya Binadamu, Wanyama na Mazingira kwa kuzingiatia msingi wa ushahidi kisera** | | | | | |
| **Lengo mahsusi** | **Mkakati** | **Shabaha** | **Kazi** | **Kiashirio** | **Namna ya kupima kiashirio** |
| 4.1 Kuongeza wingi na ubora wa tafiti za Afya Moja | 4.1.1 Shirikisha wadau husika kuandaa ajenda ya utafiti wa Afya Moja | 4.1.1.1 Tambua vipaumbele vya utafiti wa Afya Moja kufikia Juni 2023. | Tambua wadau wa Afya Moja | - Idadi ya wadau wa Afya Moja walotambuliwa | - Idadi ya wadau wa Afya Moja |
| | | | Fanya uainishaji wa wadau wa Afya Moja<br><br>Anzisha Vikundi kazi vya Kitaalamu ili kubainisha vipaumbele vya utafiti wa Afya Moja | -Wadau walioainishwa<br><br>Idadi ya Vikundi kazi vya Kitaalamu vilivyoanzishwa | -Wadau walioainishwa<br><br>Kuwepo kwa hadidu za rejea za Vikundi kazi vya Kitaalamu |
| | | | Endesha Warsha ili kuandaa ajenda ya kitaifa ya utafiti kwenye Afya Moja | Idadi ya warsha zilizoendeshwa<br><br>Idadi ya ajenda za kitaifa za utafiti wa Afya Moja zilizoandaliwa | Ripoti ya warsha |
| | | 4.1.1.2 Wianisha ajenda za utafiti za Kitaasisi na zile za kitaifa kwenye Afya Moja kufikia Juni 2023 | Hamasisha taasisi kuwianisha ajenda zao za utafiti na ajenda za kitaifa za utafiti wa Afya Moja | Idadi ya mikutano ya uhamasishaji iliyoendeshwa | - Ripoti za mikutano ya uhamasishaji |
| | | 4.1.1.3 Hamasisha miradi shirikishi ya utafiti miongoni mwa wadau wa utafiti wa | Endesha warsha za mapitio kuwianisha ajenda za utafiti kisekta na zile za kitaifa kwenye Afya Moja | - Idadi ya nyaraka zilizopitiwa<br>-Ajenda za utafiti | -Nakala zilizoandaliwa na kuchapwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Afya Moja | | kwenyeAfya Moja zilizoandaliwa na kuwianishwa na za Kitaifa | |
| | 4.1.2 Hamasisha na dumisha miradi shirikishi ya utafiti miongoni mwa wadau wa utafiti wa Afya Moja | 4.1.2.1 Andaa na dumisha orodha ya rasilimali zilizopo za utafiti wa Afya Moja kufikia Juni 2027 | Andaa orodha ya rasilimali za utafiti zinazopatikana kwenye Afya Moja | -Kuwepo kwa orodha moja ya rasilimali za utafiti wa Afya Moja. | -Orodha ya rasilimali za utafiti wa Afya Moja |
| | | 4.1.2.2 Andaa mapendekezo shirikishi ya kipaumbele kwenye Afya Moja miongoni mwa taasisi shiriki kufikia Juni 2027. | Unda Vikundi vya Utafiti ili kuitikia wito mbalimbali wa utafiti kwenye Afya Moja. | -Idadi ya mapendekezo ya utafiti shirikishi ya Afya Moja yaliyoandaliwa na kuwasilishwa kwa ufadhili<br>-Idadi ya miradi inayoendelea ya Afya Moja<br>-Idadi ya mikataba ya ushirikiano iliyosainiwa<br>-Idadi ya vikundi vya utafiti vilivyoanzishwa hivi karibuni vinavyoshughulikia Afya Moja | - Mawasiliano na wafadhili<br><br>-Mikataba ya Ushirikiano iliyosainiwa<br><br>-Mikabaa ya ufadhili iliyosainiwa |
| | 4.1.3Tumia majukwaa yaliyopo na andaa majukwaa mapya kwaajili ya kusambaza matokeo ya utafiti wa Afya | 4.1.3.1 Anzisha jukwaa jipya la utafiti wa Afya Moja kufikia Juni 2027<br><br>4.1.3.2 Ongeza ushiriki wa watafiti wa Afya Moja kwenye | i. Andaa Mkataba wa makubaliano hwaajili ya jukwaa la utafiti wa Afya Moja<br>ii. Sajili jukwaa jipya la utafiti kwenye afya moja kwenye Mamlaka husika za udhibiti. | -Mkataba wa makubaliano ulioandaliwa<br><br>-Jukwaa la watafiti wa Afya Moja lililozinduliwa<br><br>- Cheti cha usajili wa | -Idadi ya Mikataba ya Makubaliano yaliyosainiwa<br>- Cheti cha usajili<br>- Ripoti ya uzinduzi<br>- Ripoti za warsha na mikutano |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Moja | majukwaa ya utafiti (k.m., TPHA, TVA, TAWIRI, NIMR n.k.) ili kusambaza matokeo ya utafiti wa Afya Moja ifikapo Juni 2027. | iii. Zindua na endesha jukwaa la utafiti wa Afya Moja lililoundwa | jukwaa<br>-Idadi ya vikundi vya utafiti wa afya moja vilivyohamasishwa | |
| | | | iv. Hamasisha vikundi mbalimbali vya utafiti wa Afya Moja kusambaza matokeo ya utafiti katika majukwaa mbalimbali. | -Idadi ya mawasilisho ya utafiti yaliyosambazwa kwa mwaka | |
| | | | v. Wasilisha matokeo ya utafiti wa Vikundi mbalimbali vya Utafiti wa Afya Moja katika majukwaa ya utafiti | -Idadi ya warsha na mikutano | |
| | 4.1.4 Tumia teknolojia na uvumbuzi kutatua changamoto za Afya Moja | 4.1.4.1 Ongeza idadi ya teknolojia na uvumbuzi ili kukabiliana na changamoto za Afya Moja ifikapo Juni 2027. | i. Tambua, pitia upya na changua teknolojia na uvumbuzi unaoendana na shughuli za Afya Moja | -Idadi ya teknolojia na uvumbuzi uliotambuliwa, kupitiwa upya na kuchaguliwa | -Orodha ya teknolojia na uvumbuzi unaotumika |
| | | | ii. Sambaza na tumia teknolojia na uvumbuzi zilizoaninishwa kutatua changamoto za Afya Moja | -Idadi ya teknolojia na uvumbuziunaotumika. | |

| Nguzo ya Mkakakati Na. 5: Uelewa, Utetezi na Mawasiliano | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Mkakati: Kuongeza Uelewa, utetezi na mawasiliano kwa wataalamu wa Afya Moja, watunga sera na Jamii** | | | | | |
| **Lengo mahsusi** | **Mkakati** | **Shabaha** | **Kazi** | **Kiashirio** | **Namna ya kupima kiashirio** |
| 5.1 Kuongeza uelewa kuhusu Afya Moja katika ngazi ya jamii | 5.1.1 Andaa na sambaza nyenzo za Habari, mawasiliano na elimu kwa ajili ya kuongeza uelewa kwa wadau mbalimbali wa Afya Moja | 5.1.1.1 Andaa na chapisha nyenzo za uhamasishaji wa Habari, mawasiliano na elimu kwa ajili ya kuongeza uelewa kuhusu Afya Moja ifikapo 2027. | i. Fanya mkutano wa awali ili kubaini wadau na panga warsha ya kuandaa nyenzo za uhamasishaji wa Habari, mawasiliano na elimu kuhusu Afya Moja. | -Mikutano iliyofanyika | - orodha ya Walioshiriki<br>-Muhtasari wa mikutano |
| | | | ii. Fanya warsha 2 za kuandaa rasimu ya nyenzo za uhamasishaji wa Habari, mawasiliano na elimu kuhusu Afya Moja. | Aina na Idadi ya nyenzo zilizoandaliwa | Ripoti za warsha |
| | | | iii. Fanya warsha 1 kwa ajili ya kukamilisha nyenzo za uhamasishaji wa Habari, mawasiliano na elimu kuhusu Afya Moja. | -Aina na idadi ya nyenzo zilizoandaliwa na kukamilika | -Kuwepo kwa ain a na idadi ya nyenzo |
| | | | iv. Chapisha nyenzo za kuhamasisha Habari, mawasiliano na elimu kuhusu Afya Moja | Nyenzo za Uhamasishaji zilizochapishwa | Kuwepo kwa aina za nyenzo zilizochapishwa |
| | | 5.1.1.2 Sambaza nyenzo za uhamasishaji wa Habari, mawasiliano na elimu kuhusu | i. Sambaza nyenzo za uhamasishaji wa Habari, mawasiliano na elimu kuhusu Afya Moja kwa mikoa na wilaya | -Idadi ya mikoa na wilaya iliyosambaziwa nyenzo za Habari, mawasiliano na elimu kuhusu Afya Moja | - Taarifa za makabidhiano ya nyenzo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Afya Moja ifikapo 2027 | ii. fanya mikutano mitano ya usambazaji kwa watoa uamuzi kitaifa na kimkoa | -Idadi ya mikutano ya usambazaji iliyofanyika katika ngazi mbalimbali | -Ripoti ya Usambazaji |
| | | | iii. Fanya warsha 20 za usambazaji kwa wadauwa Afya Moja | -Idadi ya wadau wanaoshiriki katika warsha za usambazaji<br>-Idadi ya mikutano iliyofanyika | - Orodha ya washiriki<br>-Taarifa za warsha |
| | Jenga uelewa kwa jamii a na vyombo vya habari kuhusu Afya Moja kupitia vyombo vya habari na majukwaa mengine | 5.1.1.1 Fanya shughuli za uhamasishaji wa Afya Moja wakati wa maadhimisho ya kimataifa na kitaifa (kama vile Wiki ya Afya Moja Duniani Wiki ya usugu wa vimelea vya magonjwa kwa dawa, Siku ya Kichaa cha mbwa Duniani, Siku ya Mazingira Duniani na maadhimisho mengineyo) ifikapo 2027. | i. Andaa kalenda ya kila mwaka ya siku za maadhimisho ya Afya Moja duniani na kitaifa. | - Kuwepo kwa Kalenda ya siku za maadhimisho ya Afya Moja ya kimataifa na kitaifa<br>-Idadi ya siku ambazo shughuli za uhamasishaji wa Afya Moja zilifanyika<br>-Idadi ya mikoa na wilaya zilizoadhimisha siku siku ya Afya moja | -Kalenda<br>-Taarifa ya tukio |
| | | | ii.. Wezesha wadau kufanya uhamasishaji wa Afya Moja wakati wa maadhimisho Afya Moja ya kitaifa na kimataifa | | |
| | | 5.1.1.2 Fanya mikutano/kampeni za uhamasishaji wa Afya Moja katika ngazi ya jamii na wadau mbali mbali ifikapo 2027. | Wezesha wadau kufanya mikutano/kampeni za uhamasishaji wa Afya Moja. | -Idadi ya mikutano/kampeni zinazofanywa na wadau mbalimbali<br>-Idadi ya wadau walishiriki wakati wa | -Muhtasari wa mikutano/ ripoti ya kampeni<br>-Daftari za mahudhurio ya washiriki |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mikutano/kampeni za uhamasishaji kwa kila wilaya | |
| | | 5.1.1.3 Fanya mikutano ya kuwashirikisha na kuwahamasisha wanahabari kuhusu Afya Moja ifikapo 2027 | i.Fanya mijadala na waandishi wa habari kuhusu Afya Moja | -Idadi ya mijadala ya vyombo vya habari iliyofanyika kuhusu Afya Moja | Ripoti ya uhamasishaji/ushiriki |
| | | | ii.Endesha warsha za uhamasishaji wa vyombo na waandishi wa habari | -Idadi ya warsha za uhamasishaji zilizofanyika kuhusu Afya Moja | Ripoti ya vyombo vya Habari Vilivyoshiriki |
| | | | iii. Ushirikishwaji wa wanahabari katika shughuli za Afya Moja. | -Aina za vyombo vya habari iliyohamasishwa kuhusu Afya Moja<br>-Idadi ya vyombo vya habari vilivyoshiriki | Orodha ya vyombo vya Habari na waandishi wa habari |
| 5.2 Kuimarisha utetezi kuhusu mbinu ya Afya Moja kwa watunga sera, watoa uamuzi na wadau wengine | 5.2.1 Pata uungwaji mkonona usaidizi wa wa kiwango cha juu kwa shughuli za Afya Moja kutoka kwa watunga sera, watoa maamuzi na wadau wengine. | 5.2.1.1 Fanya mikutano/warsha ya utetezi kwa watunga sera, watoa uamuzi na wadau wengine katika ngazi ya kitaifa na ya chini ifikapo 2027. | Fanya mikutano/warsha na watunga sera, watoa uamuzi na wadau wengine. | -Idadi ya mikutano /warsha zilizofanyika na aina ya wadau walioshiriki<br><br>-Idadi ya mikutano na/au warsha zilizofanywa na wadau katika ngazi mbalimbali (kitaifa, mkoa, wilaya) | -Miniti za mikutano<br>- Ripoti za warsha<br>- Orodha ya washiriki |
| | 5.2.2 Andaa, sambaza na tekeleza Utetezi wa Afya Moja | 5.2.2.1 Andaa Mwongozo wa Utetezi wa Afya Moja ifikapo 2027 | i. Fanya mikutano ya maandalizi ya kuandaa miongozo ya utetezi | -Idadi ya mikutano ya maandalizi iliyofanyika | -muhtasari ya mkutano |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | ii. Fanyawarsha 2 za kuandaa mwongozo wa Utetezi wa wa Afya Moja | Idadi ya warsha zilizofanyika | -Ripoti za warsha |
| | | | iii. Fanya warsha 1 ya kuandaa Mwongozo wa utetezi Afya Moja<br><br>i. Chapisha Mwongozo wa Afya Moja | -Nakala ya mwongozo wa utetezi wa Afya Moja | -Nakala iliyochapwa |
| | | | i. Sambaza Mwongozo wa utetezi Afya Moja | Idadi ya mikoa na Wilaya zilizosambaziwa miongozo | Taarifa ya mapokezi ya miongozo |
| | | 5.2.2.1 Andaa Zana za Utetezi wa Afya Moja ifikapo 2027 | i.Fanya mikutano ya maandalizi ya kuandaa Zana ya Utetezi wa Afya Moja | -Idadi ya mikutano ya maandalizi iliyofanyikai | -Muhutasari wa mikutano |
| | | | ii. Fanya warsha 2 za kuandaa Zana za Utetezi wa Afya Moja | -Idadi ya warsha zilizofanyika | Ripoti za warsha |
| | | | iii. Fanya warsha 1 ya kuandaa Zana za Utetezi wa Afya Moja | -Rasimu ya mwisho ya Zana za utetezi wa Afya Moja | Kuwepo kwa rasimu ya mwisho wa zana |
| | | | iv. Chapisha Zana ya Utetezi wa Afya Moja | Idadi ya nakala za utetezi zilizochapishwa | Kuwepo kwa waakala za utetezi |
| | | 5.2.2.2 Sambaza Mwongozo wa Utetezi wa Afya Moja ifikapo 2027 | i. Sambaza miongozo ya Utetezi wa Afya Moja kwa mikoa na wilaya | -Idadi ya mikoa na wilaya ambapo *miongozo ya Utetezi wa Afya Moja imesambazwa* | -Taarifa ya usambazaji |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | ii. Fanya kongamano la usambazaji wa mwongozo wa utetezi wa Afya Moja. | -Idadi ya wadau wanaoshiriki katika kongamano la usambazaji wa Miongozo ya Utetezi wa Afya Moja | - Ripoti ya usambazaji |
| | | 5.2.2.3 Sambaza Zana ya Utetezi wa Afya Moja ifikapo 2027 | i. Sambaza zana za Utetezi wa Afya Moja kwa mikoa na wilaya | -Idadi ya mikoa na wilaya ambapo Zana za Utetezi wa Afya Moja imesambazwa | -Usambazaji wa vifaa vilivyokabidhiwa kwa mikoa na wilaya |
| | | | ii. Fanya warsha/semina za usambazaji wa zana za Utetezi wa Afya Moja | -Idadi ya wadau wanaoshiriki katika warsha/semina za uenezaji wa zana za Utetezi wa Afya Moja | - Ripoti ya usambazaji<br>-Daftari la mahudhurio ya washiriki |
| 5.3 Kuimarisha mifumo ya mawasiliano na kujenga uwezo miongoni mwa wadau wakuu wa Afya Moja katika ngazi zote | 5.3.1 Andaa na sambaza mkakati wa Mawasiliano wa Afya Moja. | 5.3.1.1 Andaa Mkakati wa Mawasiliano wa Afya Moja ifikapo 2027 | i. fanya mikutano ya awali ya kuandaa Mkakati wa Mawasiliano wa Afya Moja | -Idadi ya mikutano ya maandalizi iliyofanyika | -Ripoti za mikutano |
| | | | ii. Fanya warsha 2 za kuandaa Mkakati wa Mawasiliano wa Afya Moja | -Idadi ya warsha/semina zilizofanyika | Ripoti za mikutano na warsha |
| | | | iii. Fanya warsha 1 kukamilisha Mkakati wa Mawasiliano wa Afya Moja | Nakala ya mkakati uliokamilika | -orodha ya washiriki<br>-Taarifa ya warsha |
| | | | iv. Chapisha Mkakati wa Mawasiliano wa Afya Moja | Idadi na nakla za Mkakati wa mawasiliano zilizochapishwa | Nakala za machapisho |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 5.3.1.2 Sambaza mkakati wa Mawasiliano kupitia warsha/semina ifikapo 2027 | Zindua mkakati wa mawasiliano wa Afya Moja | -Idadi ya wadau waliohudhuria uzinduzi wa mkakati wa mawasiliano wa Afya Moja | -Ripoti ya Uzinduzi |
| | | | ii. Fanya mikutano mitano ya usambazaji wa Mkakati wa Mawasiliano wa Afya Moja | --Idadi ya wadau walioshiriki katika usambazaji wa mkakati wa mawasiliano wa Afya Moja<br>-Idadi ya wadau walioshiriki katika mikutano ya usambazaji | -Orodhaya washiriki |
| | | | i. Sambaza mkakati wa mawasiliano wa Afya Moja kwa wadau | Idadi ya nakala za mikakati ya mawasiliano ya Afya Moja iliyosambazwa kwa wadau | Taarifa ya usambazaji |
| | 5.3.2 Andaana endeshamfumo wa data na taarifa za Afya Moja katika ngazi zote | 5.3.2.1 Andaa tovuti maalum ya data na taarifa za Afya Moja ifikia 2027 | i. Fanya mikutano ya kitaalamu ya kuandaa tovuti | - Mikutano iliyofanyika | -Ripoti za mikutano |
| | | | ii. Shirikisha mshauri elekezi wa kuandaa tovuti ya mtandao wa Afya Moja | -Mikataba wa Mshauri elekezi na hadidu za rejea | -<br>-Mkataba uliosainiwa |
| | | 5.3.2.2 Wezesha | Nunua programu ya tovuti | Programu iliyopakiwa | Nyaraka za manunuzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ovuti kupokea na kuhifadhi data na taarifa za Afya Moja ifikapo 2027 | | | |
| | | | | | |
| **Nguzo ya Kimkakati Na. 6 – Mafunzo na Elimu** | | | | | |
| **Lengo: Kuimarisha mafunzo na elimu kuhusu Mbinu yaAfya Moja kwa wataalamu walioko vyuoni na walioajiriwa katika sekta ya afya ya binadamu, wanyama na mazingira.** | | | | | |
| **Lengo mahsusi** | **Mkakati** | **Shabaha** | **Kazi** | **Kiashirio** | **Namna ya kupima kiashirio** |
| 6.1 Kuongeza maarifa na ujuzi kuhusu ya Mbinu ya Afya Moja kupitia mafunzo ya wataalamu walioko vyuoni na walioajiriwa kuanzia ngazi ya taifa hadi wilaya. | 6.1.1 Shirikisha taasisi za mafunzo na elimu, Wizara za Kisekta, Mamlaka ya Udhibiti wa Mafunzo na Taaluma katika kusaidia mafunzo jumuishi ya Afya Moja. | 6.1.1.1 Andaa mkutano mmoja, wa Afya Moja unaohusisha Taasisi za Mafunzo na Elimu, Wizara za Kisekta na Mamlaka ya Udhibiti wa Mafunzo na Taaluma kila mwaka. | i. Andaa Mkutano Moja, wa Afya Moja unaohusisha taasisi za Mafunzo na Elimu, Wizara za Kisekta na Mamlaka ya Udhibiti wa Mafunzo na Taaluma | •Idadi ya mkutano ulioandaliwa<br><br>Idadi ya washiriki na taasisi zilizohusishwa kwenye mkutano ulioandaliwa | Ripoti za Mkutano / minitisi<br>- Orodha ya mahudhurio ya washiriki<br>-Ripoti za kazi iliyofanyika |
| | | | ii. Endesha mkutano wa kila mwaka wa Afya Moja unaohusisha Wizara za Kisekta na , taasisi za mafunzo na elimu kuhusu shughuli za mafunzo na elimu ya mbinu ya Afya Moja | | |
| | | | iii. Endesha mkutano wa kila mwaka wa Afya Moja unaohusisha mamlaka za udhibiti taaluma na vyama vya kitaaluma kwa shughuli za mafunzo na elimu ya mbinu ya Afya Moja. | Idadi ya washiriki na Mamlakai zilizohusishwa kwenye mkutano ulioandaliwa | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 6.1.1.2 Tambua Mapengo ya mbinu ya Afya Moja kufikia Juni 2023 | i. Andaa Mkutano wa kubaini mapungufu ya mbinu ya Afya Moja. | •Idadi ya mikutano na orodha ya mapungufu yaliyoibuliwa | •Ripoti za mikutano<br>•Orodha ya washiriki<br>•Ripoti ya mapengo (gap) |
| | | | ii. Endesha Mkutano wa kiufundi ili kubaini mapungufu ya mbinu ya Afya Moja. | | |
| | | 6.1.1.3 Mapengo ya mbinu ya Afya Moja yaliyobainika kupitiwa upya na kujumuishwa katika mitaala mipya ya mafunzo kufikia Juni 2023. | i. Panga Mkutano wa Kitaalamu wa kupitia upya mitaala ya mafunzo na kujumuisha mapungufu yaliyobaikia kwenye mbinu ya Afya Moja. | •Idadi ya mitaala mipya inayojumuisha mapungufu yaliyobainika | •MiRipoti za mikutano<br>•Washiriki waliosajiliwa<br>•Ripoti ya mapengo (gaps)<br>•Mitaala iliyopitishwa na kujumuisha mapengo (gaps) ya Afya Moja |
| | | | ii. Endesha Mkutano wa Kitaalamu ili kupitia upya mitaala ya mafunzo na kujumuisha mapengo yaliyobainika ya mbinu ya Afya Moja. | | |
| | | | Sambaza mitaala ya mafunzo iliyopitiwa upya na kifurushi cha mafunzo cha Afya Moja. | | |
| | | 6.1.1.4 Fanya Mafunzo ya mbinu ya Afya Moja kwa walimu wa washiriki wa mafunzo kufikia Juni 2024 | i. Andaa Vifaa vya Mafunzo ya mbinu ya Afya Moja kwa Walimu wa Washiriki wa mafunzo | •Idadi na aina ya vifaa vya mafunzo ya mbinu ya Afya Moja vilivyoandaliwa<br>•Idadi na aina ya vifaa vya mafunzo ya walimu wa washiriki wa mafunzo vilivyonunuliwa<br>•Idadi ya warsha za | •Ripoti ya mafunzo ya walimu wa washiriki wa mafunzo<br>•Orodha ya Walimu wa Washiriki wa mafunzo.<br>Orodha ya vifaa vya mafunzo |
| | | | ii. Nunua vifaa vya mafunzo kwa ajili ya Mafunzo ya Wakufunzi (ToT) kuhusu mbinu ya Afya Moja | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | iii. Endesha Mafunzo ya Walimu wa Washiriki wa mafunzo ya mbinu ya Afya Moja | mafunzo na walimu wa washiriki wa mafunzo<br>•Asilimia ya ufanisi wa warsha ya mafunzo ya walimu wa washiriki wa mafunzo | vilivyonunuliwa |
| | | | iv. Tathmini ya ufanisi wa mafunzo ya walimu wa washiriki wa mafunzo ya mbinu yaAfya Moja | | |
| | | 6.1.1.5 Endesha Mafunzo kuhusu Mbinu ya Afya Moja kwa wanafunzi 3450 walioko vyuoni na wataalamu walioajiriwa 2000 kufikia Juni 2027. | i. Andaa mpango wa mafunzo mbinu ya Afya Moja) kwa wanafunzi 3450 walioko vyuoni na wataalamu walioajiriwa 2000 | •Mpango wa mafunzo ulioandaliwa kwa makundi yote mawili<br>Idadi na aina ya vifaa vya mafunzo ya walimu wa washiriki wa mafunzo vilivyonunuliwa<br>Idadi ya warsha za mafunzo na wanafunzi walipopata mafunzo<br>Idadi ya warsha za mafunzo na wataalamu walioajiriwa waliopata mafunzo<br>Asilimia ya ufanisi wa warsha ya mafunzo ya makundi yote mawili | •Ripoti ya mafunzo kwa wanafunzi kabla ya kuingia kazini na wanafunzi wafanyakazi waliopo kazini.<br>•Wanafunzi waliosajiliwa |
| | | | iiNunua vifaa vya mafunzo ya mbinu ya Afya Moja kwa ajili ya wanafunzi 3450 walioko vyuoni na wataalamu walioajiriwa 2000. | | |
| | | | iii. Endesha mafunzo kuhusu mbinu ya Afya Moja kwa wanafunzi 3450 walioko vyuoni | | |
| | | | iv. Endesha mafunzo juu ya mbinu ya Afya Moja kwa wataalamu walioajiriwa 2000. | | |
| | | | v. Tathmini ufanisi wa mafunzo ya mbinu ya Afya Moja kwa wanafunzi 3450 walioko vyuoni na wataalamu walioajiriwa 2000 | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 6.1.1.6 Andaa kozifupi tano za mafunzo ya kujiendeleza ya wataalamu walioajiriwa kuhusu Mbinu ya Afya Moja kufikia Juni 2027 | Andaa kozi fupi tano za mafunzo ya kujiendeleza kuhusu mbinu ya Afya Moja kwa wataalamu walioajiriwa<br>Nunua vifaa vya mafunzo ya kujiendeleza kuhusu mbinu ya Afya Moja<br>Endesha angalau programu moja iliyoandaliwa ya fani na sekta mbalimbali kuhusu mbinu ya Afya Moja | •Asilimia ya ya kozi zilizoandaliwa<br>•<br>Idadi na aina ya vifaa vya mafunzo vilivyonunuliwa<br>Idadi ya programu za mafunzo ya kujiendeleza ya mbinu ya Afya Moja zilizotekelezwa | •Kuwepo kwa mitaala ya kozi zilizoandaliwa<br>•Idadi ya mitaala iliyoandaliwa<br>Orodha ya vifaa vyaa kufundishia vilivyonunuliwa<br>•Ripoti za mafunzo<br>•Orodha ya wa washiriki |
| | 6.1.2 Andaa programu za mafunzo ya Uzoefu wa Uwandani kuhusu Afya Moja | 6.1.2.1 Andaa mmiktindo miwili ya mafunzo ya uigizaji wa matukio kwa wanafunzi walioko vyuoni kufikia Juni, 2027 | i. Andaa mitinndo miwili ya mafunzo ya uigizaji wa matukio kwa wanafunzi walioko vyuoni<br>ii. Endesha mafunzo kwa kutumia mitindo ya uigizaji wa matukio | •*Idadi ya mitindo ya mafunzo ya wanafunzi iliyoandaliwa* | •Mifano ya uigizaji wa mafunzo<br>• Ripoti ya kazi |
| | | 6.1.2.2 Anzisha Vilabu Mia (100) vya Wanafunzi vya Ubunifu wa mbinu ya Afya Moja, kwa katika taasisi za mafunzo na elimu kufikia Juni 2027. | i. Endesha mikutano ya uhamasishaji kwa ajili ya kuanzisha Vilabu vya Ubunifu vya Mbinu ya Afya Moja.<br>ii. Anzisha Vilabu 100 vya Wanafunzi vya Ubunifu wa Mbinu ya Afya Moja katika taasisi za mafunzo na elimu | •<br>Idadi ya vilabu vya wanafunzi vya ubunifu vya vya mbinu ya Afya Moja vilivyoanzishwa. | •Orodha ya ya Vilabu vya Wanafunzi vya mbinu yaAfya Moja vilivyoanzishwa<br>Orodha ya wanafunzi waliojiunga kwenye vilabu<br>•Ripoti za uanzishwaji wa Vilabu vya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | iii. Simamia Vilabu vya Wanafunzi vya Ubunifu vya Mbinu ya Afya Moja (OH) katika taasisi za mafunzo na elimu | | Ubunifu vya mbinu ya Afya Moja |
| | | 6.1.2.3 Unda Mtindowa wanafunzi wa mafunzo na huduma za kudhibiti/kutokomeza viwango vya magonjwa ya kuambukiza kila mwaka. | i. Unda mtindo wa wanafunzi wa mafunzo na huduma za kudhibiti/ kutokomeza viwango vya magonjwa ya kuambukiza kila mwaka<br>ii. Endesha semina ya uhamasishaji kwa wanafunzi kuhusu mitindo ya mafunzo na huduma za kudhibiti/kutokomeza viwango vya magonjwa ya kuambukiza kila mwaka<br>i. Tumia mtindo wa wanafunzi wa mafunzo na huduma za kudhibiti kutokomeza viwango vya magonjwa ya kuambukiza kila mwaka | •Idadi ya mitindo ya mafunzo na huduma za kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya kuambukiza iliyoundwa | Kuwepo kwa mitindo ya mafunzo na huduma za kudhibiti na kutokomeza magonjwa<br><br>•Ripoti za uundaji wa mitindo ya mafunzo na huduma za kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya kuambukiza |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 6.1.2.4 Anzisha Kanda tisa za mbinu ya Afya Moja kwenye mikoa kushiriki kwenye maazimisho ya ya matukio ya Afya Moja (k.m. Wiki ya Uhamasishaji ya Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi hya Dawa Duniani, Siku ya Kichaa cha Mbwa) kwenye ngazi ndogo za kitaifa kufikia Juni, 2027. | i. Andaa Andiko la Dhana ya kuanzisha Kanda za Afya Moja kwenye mikoa kushirikii katika maadhimisho ya matukio ya Mbinu za Afya Moja (k.m. Wiki ya Uhamasishaji ya Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi hya Dawa Duniani, Siku ya Kichaa cha Mbwa, Siku ya Mazingira), katika ngazi ndogo za kitaifa. | •Idadi ya Kanda za Afya Moja kwenye Mikoa iliyoanzishwa | •Andiko la Dhana ya kuanzisha Kanda<br>•Kanda za Afya Moja zilizoanzishwa<br>•Ripoti za uanzishwaji wa Kanda |
| | | | ii. Anzisha Mpango Kazi wa kuanzisha Kanda 9 za Afya Moja kushiriki katika maazimisho ya matukio ya mbinu ya Afya Moja (k.m. Wiki ya Uhamasishaji ya Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi hya Dawa Duniani, Siku ya Kichaa cha mbwa, Siku ya Mazingira), katika ngazi ndogo ya kitaifa. | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | iii. Anzisha Kanda 9 za Afya Mojakwenye Mikoa kushiriki katika maazimisho ya matukio ya Afya Moja (k.m. Wiki ya Uhamasishaji ya Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi hya Dawa Duniani, Siku ya Kichaa cha mbwa, Siku ya Mazingira), katika ngazi ndogo ya kitaifa. | | |
| | 6.1.3 Imarisha mafunzo ya wanafunzi yanayozingatia Mbinu ya Afya Moja. | 6.1.3.1 Andaa mitaala ya mafunzo ya marejeo ya Afya Moja kufikia Juni 2023. | i. Fanya mkutano wa kitaalamu wa kuandaa mitaala ya mafunzo ya ya marejeo ya Afya Moja. | •Idadi ya mitaala ya mafunzo ya marejeo ya Afya Moja iliyotengenezwa/kukaguliwa. | •Kuwepo kwa mitaala ya marejeo ya Afya Moja<br>•Ripoti za uandaaji wa Mitaala ya marejeo ya Afya Moja |
| | | | ii. Sambaza mitaala ya mafunzo ya marejeo ya Afya Moja. | | |
| | | | iii. Fanya mafunzo ya marejeo ya Afya Moja kwa kutumia mitaala iliyotengenezwa | | |
| | | 6.1.3.2 Andaa miongozo minne (4) ya kufundishia mafunzo ya marejeo ya Mbinu ya Afya Moja kwa wataalamu walioko vyuoni na walioajiriwa kufikia Juni 2027. | iAndaa bajeti ya kuandaa miongozo minne (4) ya Kufundisha kwa kutumia mitaala ya marejeo ya mbinu ya Afya Moja, kwa wanafunzi walioko Vyuo Vikuu, na Taasisi za Elimu ya Ufundi. | •Idadi ya Miongozo ya ya kufundishia iliyoandaliwa. Idadi ya Taasisi zilizoshirikishwa | •Kuwepo kwa Miongozo ya Kufundishia<br>•Ripoti ya uandaaji wa Miongozo ya Kufundisha Afya Moja vitabu, mwongozo, makabrasha mengine |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | ii. Kusanya rasilimali kwa ajili ya kuandaa Miongozo minne (4) ya kutumia mitaala ya marejeo ya mbinu ya Afya Moja kwa ajili ya wanafunzi walioko Vyuo Vikuu, na Taasisi za Elimu ya Ufundi.i. | | (compendia)<br>•Ripoti za unadaaji wa mitaala na miongozo ya kufundishia |
| | | | iii. Tambua utaratibu maalum (ushauri, tumia wataalamu nje ya taasisi, ushiriki wa Taasisi za Elimu, na mpango wa Afya Moja) wa kuandaa Miongozo minne (4) ya Kufundisha kwa kutumia mitaala ya marejeo ya Afya Moja. | | |
| | | 6.3.3 Andaa Vitabu vya Mbinu ya Afya Moja {vitabu vilivyochapishwa & vitabu vya kielektroniki mwongozo mmoja (1) na Vitabu Muhtasari/kompedia saba (7) kwa ajili ya | i. Andaa mpango wa gharama ya kuandika vitabu vya mbinu ya Afya Moja {Vitabu vilivyochapishwa & Vitabu vya Elektroniki) mwongozo mmoja (1) na vitabu muhtasari/kompedia saba (7) kwa wataalamu walio vyuoni na walioajiriwa. | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wataalamu walio vyuoni na walioajiriwa kufikia Juni 2027. | ii. Kusanya rasilimali kwa ajili ya kuandika vitabu vya Mbinu ya Afya Moja {Vitabu vilivyochapishwa & Vitabu vya kielektroniki mwongozo/ mmoja (1) na vitabu muhtasari/kompendia saba (7) kwa ajili ya wataalamu walio vyuoni na walioajiriwa. | | |
| | | | iii. Tambua utaratibu maalum (ushauri, tumia wataalamu nje ya taasisi, , ushiriki wa Taasisi, mpango wa Afya Moja) wa kuandika {(vitabu vilivyochapishwa na vitabu vya kielektroniki)}, mwongozo mmoja (1) na vitabu muhtasari/kompedia saba (7) kwa wataalamu walioko vyuoni na walipajiriwa | | |
| | | | iv. Wezesha uandaaji wa vitabu vya Mbinu ya Afya Moja vilivyochapishwa na vya kielektroniki, mwongozo mmoja (1) na vikgabu muhtasari/kompendia saba (7) kwa wataalamu walioko vyuoni na walipajiri.. | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | v. Sambaza vitabu vilivyoandikwa vya Mbinu ya Afya Moja {vilivyochapishwa na vya kielektroniki, mwongozo mmoja (1) na vitabu muhtasari/kompedia saba (7) kwa wataalamu walioko vyuoni na walipajiri. | | |

## 4.0 MFUMO WA KUTOA MATOKEO

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inatoa msingi wa jinsi afua mbalimbali zinavyohusishwa na Malengo na jinsi yatakavyofuatiliwa; ni aina gani ya mapitio yatafanywa kuhusu Mzunguko wa Upangaji Mkakati; ni aina gani za tathmini zitafanywa ili kuonesha kwamba afua ama zimeongoza au zimesababisha kupatikana kwa matokeo yaliyokusudiwa; na jinsi maendeleo ya afua mbalimbali yatakavyotolewa taarifa.

### 4.2 Mlolongo wa Matokeo

Mchanganyiko wa malengo na shabaha katika Mpango Mkakati,shughuli na nyenzo katika Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) huunda mlolongo wa matokeo ya Afya Moja. Dhana ya msingi ni kwamba, kuna uhusiano wa sababu katika vipengele mbalimbali vya mlolongo wa matokeo ya Afya Moja . Nyenzo, ambazo ni, matumizi ya rasilimali itasababisha mafanikio ya shughuli, ambayo yatachangia kupatikana kwa matokeo.

### 4.3 Matriksi ya Mfumo wa Matokeo

Matriksi hii ina malengo, matokeo yanayotarajiwa na viashirio. Inaonesha jinsi malengo yatavyofikiwa na jinsi matokeo yatavyopimwa. Viashirio vilivyo kwenye matriksi vitatumika kufuatilia maendeleo ya kufikia matokeo na malengo. Matriksi ya Mfumo wa Matokeo imefafanuliwa kwenye jedwali Na.3.

### Jedwali Na. 3: Mpango wa Utoaji wa Taarifa

| NGUZO ZA KIMKAKATI | MSIMBO WA LENGO | LENGO MAHUSUSI | MATARAJIO | VIASHIRIO |
|---|---|---|---|---|
| URATIBU | A | 1.1 Imarisha uwezo wa utendaji kazi wa sehemu ya Afya Moja | i. Ushirikiano ulioboreshwa kati ya sehemu ya Afya Moja na Wizara za kisekta | Ushirikishanaji wa taarifa miongoni mwa sekta.<br><br>Idadi ya mikutano ya pamoja kati ya sekta na wizara<br><br>Idadi ya wafanyakazi wa sehemu ya Afya Moja na waratibu viungo waliopewa mafunzo<br><br>Ripoti ya tathmini ya utendaji ya vikundi kazi vya kitaalamu |
| | | | ii. Utendaji ulioboreshwa wa wafanyakazi wa sehemu ya Afya Moja | |
| | | | iii. Ushirikiano na mawasiliano kati ya sekta za Afya Moja yaliyoboreshwa | |
| | | | iv. Ufanisi ulioboreshwa wa vikundi kazi vya kitaalamu na sehemu ya Afya Moja | |
| | B | 1.2 Ongeza rasilimali ili kusaidia shughuli za Afya Moja; | i. kwa Usaidizi wa kifedha kwa mipango inayopendekezwa ya Afya Moja umeongezeka miongoni mwa sekta zote | Ongezeko la asilimia la programu zinazofadhiliwa na Afya Moja |
| | | | ii. Wafanyakazi wa kutosha walioajiriwa katika sekta zote za | Idadi ya wafanyakazi wa Afya Moja walioajiriwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Afya Moja | |
| | C | 1.2 Imarisha uhusiano wa kikazi kati ya Sehemu ya Afya Moja na majukwaa ya Afya Moja ya ndani na ya Kimataifa. | Uhusiano wa kikazi ulioboreshwa kati ya Sehemu ya Afya Moja na majukwaa ya ndani na ya kimataifa | -Idadi ya mikutano ya majukwaa ya Afya Moja ambayo wafanyakazi wa Sehemu ya Afya Moja wameshiriki<br><br>-Idadi ya shughuli za ushirikiano zilizopangwa |
| Ufuatiliaji, Utambuzi na Udhibiti | D | 2.1 Imarisha ufuatiliaji wa pamoja, wa magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na matishio mengine ya afya ya jamii katika ngazi zote. | i. Ushirikishanaji wa data za ufuatiliaji na maoni umeboreshwa katika sekta zote | Idadi ya ripoti za ufuatiliaji ambazo sekta zimeshirikishana |
| | | | ii. Ubora na wingi wa data ya ufuatiliaji na matumizi kwa ajili ya kufanya uamuzi umeboreshwa | - Idadi ya mikutano ya kila robo mwaka iliyofanywa ya kushirikishana data za ufuatiliaji<br><br>- Idadi ya data za ufuatiliaji zilizotumika kufanya uamuzi |
| | | | iii. Ushirikishwaji na ushiriki wa jamii katika ufuatiliaji na utoaji taarifa umeongezeka | Asilimia ya data za ufuatiliaji zenye ubora |
| | E | 2.2 Imarisha, zuia na dhibiti magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na | i. Utekelezaji wa mikakati ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na | Asilimia ya ongezeko la chanjo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele ya zuonotiki |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | matishio mengine ya afya ya jamii katika ngazi zote. | matishio mengine ya afya ya jamii umeimarika katika ngazi zote. | |
| | | | ii. Uwezo wa wafanyakazi katika kuzuia na kudhibiti magonjwa ya zuonotiki yaliyopewa kipaumbele, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na matishio mengine ya afya ya jamii umeboreshwa katika ngazi zote. | Idadi ya wafanyakazi waliopata mafunzo kuhusu kuzuia na kudhibiti magonjwa ya zuonotiki yaliyopewa kipaumbele, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii |
| | | | iii. Uelewa na ushiriki wa watendaji katika kuzuia na kudhibiti magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na matishio mengine ya afya ya jamii umeongezeka katika ngazi zote. | Idadi ya wafanyakazi waliopata mafunzona kuhusika katika kuzuia na kudhibiti magonjwa ya zuonotiki yaliyopewa kipaumbele, sugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matukio mengine ya afya ya jamii |
| | F | Imarisha uwezo wa utambuzi wa magonjwa ya zuonotiki yaliyopewa kipaumbele katika viwango vya kitaifa (100%), kanda, mkoa (60%) na wilaya (30%). | i. Uwezo wa maabara wa kugundua magonjwa yaliyopewa kipaumbele ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, na matishio mengine ya afya ya jamii umeboreshwa katika ngazi zote. | Idadi za maabara zenye uwezo wa kutambua magonjwa ya kipaumbele ya zuonotiki, usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na matishio mengine ya afya ya jamii |
| | | | ii. Ushirikishanaji wa taarifa za maabara miongoni mwa sekta kwa ajili ya kufanya uamuzi sahihi uboreshwa | - Idadi ya taarifa za maabara zilizoshirikishwa miongoni mwa sekta |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | iii. Hatua zilizoboreshwa za usalama na ulinzi wa kibiolojia | Idadi ya mikutano ya robo mwaka iliyofanyika ya kushirikishana data za maabara<br><br>Idadi ya vituo vinavyotekeleza usimamizi wa usalama na ulinzi wa kibiolojia<br><br>- Idadi ya vituo vyenye mwongozo wa usimamizi wa usalama na ulinzi wa kibiolojia. |
| Mifumo ya kujiandaa na kukabiliana wakati wa dharura | G | 3.1 Imarisha mifumo ya sekta mbalimbali ya kujiandaa na kukabiliana na matishio yanayoibuka na kujirudia. | Utaratibu wa mifumo ya kijiandaa na kukabiliana na matishio katika sekta mbalimbali upo katika ngazi zote | Idadi ya Uratibu wa mwitikio wa dharura katika sekta mbalimbali kuhusu matishio yanayoibuka na kujirudia. |
| | H | 3.2 Imarisha mifumo ya utendaji kazi ya sekta mbalimbali katika kujiandaa na kukabiliana na matishio yanayoibuka na yanayojirudia katika ngazi zote. | i. Idadi ya Vituo vya Utendaji vya Dharura vya sekta mbalimbali vinavyofanya kazi katika ngazi ya chini vimeongezeka | Idadi ya Vituo vya Uendeshaji vya Dharura vya sekta mbalimbali vinavyofanya kazi katika ngazi ya chini |
| | | | ii. Ushiriki wa kamati za sekta mbalimbali za kukabiliana na dharura umeboreshwakatika katika ngazi ya chini | Idadi ya mikutano ya sekta mbalimbali ya kujiandaa na kukabiliana na dharura katika ngazi ya chini |
| Utafiti na Maendeleo | I | 4.1 Ongeza kiasi na ubora wa tafiti za Afya Moja | i. Ushirikiano wa tafiti za Afya Moja ndani na nje ya Tanzania umeboreshwa | Idadi ya miradi shirikishi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ii. Ufadhili wa kuwezesha shughuli za utafiti wa Afya Moja umeongezeka | Asilimia ya mgawo wa bajeti ya fedha kwa ajili ya utafiti wa Afya Moja katika wizara husika |
| | | | iii. Teknolojia na ubunifu wa kutatua changamoto za Afya Moja (OH) umeanzishwa | Ubunifu/teknolojia mpya zilizoanzishwa |
| Uhamasishaji, Utetezi na Mawasiliano | J | 5.1 Ongeza uelewa kuhusu Afya Moja katika ngazi ya jamii | Uelewa wa wanajamii kuhusu masuala mbalimbali ya Afya Moja umengezeka | Asilimia ya wanajamii wanaoelewa masuala mbalimbali ya Afya Moja |
| | K | 5.2 Imarisha utetezi kuhusu mbinu ya Afya Moja kwa watunga sera, watoa uamuzi na wadau wengine | Kuthaminiwa kwa umuhimu wa mbinu ya Afya Moja kati ya watunga sera, watoa uamuzi na wadau wengine kumeimarika | Asilimia ya watunga sera, watoa uamuzi na wadau wengine wanaothamini mbinu ya Afya Moja |
| | L | 5.3 Imarisha mifumo ya mawasiliano na uwezo miongoni mwa wadau wakuu wa Afya Moja katika ngazi zote | Ushirikishanaji wa taarifa za Afya Moja miongoni mwa wizara za kisekta na wadau wengine husika umeimarika. | Idadi ya wizara za kisekta na wadau wengine husika wanaoshirikishana Taarifa za Afya Moja |
| Mafunzo na Elimu | M | 6.1 Ongeza maarifa, ujuzi na mazoezi kuhusu Mbinu ya Afya Moja kupitia mafunzo kwa walio kazini na mafunzo tarajali kutoka ngazi ya taifa hadi wilaya. | kwa Uelewa na kukubalika kwa Mbinu ya Afya Moja miongoni mwa watunga sera, watoa uamuzi na jamii. kumeongezeka | Uwiano wa watunga sera, watoa uamuzi na jamii yenye uelewa wa wazi na kukubali Mbinu ya Afya Moja |

## 4.4 UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 4.4.1 Ufuatiliaji na Tathmini

Kusudi la ufuatiliaji ni kuhakikisha Mpango Mkakati unatekelezwa kuendana na muda uliopangwa na iwapo itatokea kasoro yoyote hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati. Ufuatiliaji utafanyika mara kwa mara na tathmini itafanyika katika vipindi maalum vilivyopangwa. Ufuatiliaji utahusisha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za mara kwa mara kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa mpango ili kuhakikisha kwamba utekelezaji unakwenda sawa na malengo yanafikiwa. Matokeo ya tathmini yatatumika na watoa maamuzi kuchukua hatua stahiki na kwa wakati kurekebisha kasoro zilizobainishwa

### 4.4.2 Mpango wa Ufuatiliaji

